# MOFOFONOLOJIA YA NOMINO MKOPO ZA KITURKANA KUTOKA KISWAHILI

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

EDWARD EKADELI LOKIDOR

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA KUSUDI LA KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

*1702330*
UoN Thesis
2017

(2017)

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa kwa chuo kikuu chochote kile kwa mahitaji ya shahada.

.................................................. Tarehe..15/11/2017..

Mtahiniwa

Edward Ekadeli Lokidor

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

........................................................................ Tarehe..16/11/2017..

Prof. Iribe Mwangi

........................................................................ Tarehe..16/11/2017..

Dkt. Samwel M. Obuchi

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa babangu, James Lokidor, mamangu Selina Ibuya na dadangu Anne Lokidor kwa kuniauni kwa hali na mali katika harakati zangu za kusaka elimu.

**SHUKRANI**

Kwanza kabisa, ningependa kuchukua dafina hii adhimu kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rabuka kwa kunipa siha njema na kuniwezesha kukamilisha kazi hii aula. Pia ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Prof. Iribe Mwangi na Dkt. Samwel M. Obuchi kwa maelekezo na ushauri muhimu. Hakika hawakuchoka kunishauri na kunipa shime nikamilishe kazi hii. Jalali awape siha njema na baraka tele maishani.

Aidha, ningependa kuwashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili walionifunza kama vile: Prof. Rayya, Prof . Habwe, Prof. Mbatiah, Prof. Kinene, Prof. Iribe, Dkt. Zaja, Dkt Jefwa, Dkt. Mbuthia, Dkt.Swaleh na Dkt. Jerono. Maarifa niliyopata darasani yamekuwa amana kubwa kwangu hususan katika tasnia ya Kiswahili. Jalali awajalie baraka tumbi nzima maishani.

Vile vile nawashukuru wanazuo wenzangu tulioabiri nao ngalawa ya masomo hadi mwisho wa safari. Nao ni James Kimwea, Dorcas Sutta, Patrick , Tecla, Sarah, Makori, Mumo, Wakesho na Wairimu.

Mwisho kabisa, ningependa kuwashukuru waja wote walioniuni kwa njia moja au nyingine katika kuifanikisha kazi hii. Mola awabariki upeo wa kubarikiwa.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu mofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili ambapo tumechanganua mifanyiko ya kimofofonolojia ambayo nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hupitia ndipo zikubalike katika Kiturkana. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza vipengele vya fonolojia ya Kiturkana kama vile irabu, nusu-irabu, konsonanti na silabi. Utafiti huu pia ulilenga kubainisha mabadiliko ya sauti yanayokumba konsonanti na irabu za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Nadharia ya fonolojia zalishi asilia ilielekeza utafiti huu katika kubaini mifanyiko ya kimofofonolojia ambayo nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hupitia na kanuni zinazodhibiti mifanyiko hii. Tulikusanya data yetu maktabani yaani kutoka kwa Bibilia ya Kiturkana, Misali na Kamusi ya Kiingereza — Kiturkana na kuwasilisha kifonetiki na kiothografia. Utafiti huu umebaini kwamba kuna fonimu ambazo zipo katika Kiswahili lakini hazipo katika Kiturkana. Utafiti huu pia umetambua kwamba konsonanti za Kiswahili zinapokopwa na Kiturkana hupitia mabadiliko ya kifonolojia kama vile udhoofikaji, uimarikaji, udondoshaji, uchopekaji, usilimisho pamwe wa nazali na ubadala wa konsonanti ili nomino hizi zikubalike katika Kiturkana kwa lengo la kusahilisha utamkaji, kupata muundo mwafaka wa silabi na mofu ya jinsia ambayo hutumiwa kuainisha nomino za Kiturkana. Aidha, tumebaini kwamba vokali za nomino za Kiswahili zinapokopwa na Kiturkana hupitia mabadiliko ya kifonolojia kama vile udondoshaji wa irabu, uchopekaji wa irabu, ubadala wa irabu, uyeyushaji na uwiano wa irabu ili nomino za Kiswahili zikubalike katika Kiturkana ili kusahihilisha utamkaji, upatakaji wa miundo ya silabi na mofu ya nomino husika katika Kiturkana.

## MAELEZO YA ALAMA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA KATIKA KAZI HII

/ / ni mabano ya kifonetiki

→ Inabadilika na kuwa

\+ ina maana ya iliyo

\> mabadiliko

– isiyo

[ ] ni mabano ya fonimu

$ mpaka wa silabi

# mpaka wa neno

I ni irabu au vokali

K ni Konsonanti

Kons ni konsonanti

Naz ni nazali

NFZA ni Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia

# YALIYOMO

UNGAMO ........ ii

TABARUKU ........ iii

SHUKRANI ........ iv

IKISIRI ........ v

MAELEZO YA ALAMA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA KATIKA KAZI HII . vi

YALIYOMO ........ vii

SURA YA KWANZA ........ 1

1.0Utangulizi ........ 1

1.0.1 Lugha ya Kiturkana ........ 4

1.0.2Lugha ya Kiswahili ........ 5

1.1 Suala la utafiti ........ 7

1.2 Malengo ya utafiti ........ 8

1.3 Umuhimu wa utafiti ........ 8

1.4 Nadharia tete ........ 9

1.5 Upeo wa utafiti ........ 9

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........ 10

1.6.1 Maandishi ya Kijumla kuhusu ukopaji wa maneno ........ 10

1.6.2 Maandishi bayana kuhusu ukopaji ........ 13

1.7 Msingi wa nadharia ........ 20

1.7.1 Kanuni za kifonetiki ........ 22

1.7.2 Kanuni za mofolojia ........ 22

1.7.3 Kanuni za via ..... 23

1.7.4 Kanuni za Sandhi ..... 23

1.8 Mbinu za utafiti ..... 24

1.8.1 Uteuzi wa sampuli ..... 24

1.8.2 Mbinu za kukusanya data ..... 25

1.8.3 Uchanganuzi wa data ..... 25

1.8.4 Uwasilishaji wa data ..... 26

SURA YA PILI ..... 27

2.0 FONOLOJIA YA KITURKANA ..... 27

2.1 Utangulizi ..... 27

2.1.1 Fonimu za Kiturkana ..... 27

2.1.2 Fonimu za irabu za Kiturkana ..... 28

2.1.3 Fonimu za Konsonanti za Kiturkana ..... 34

2.2 Silabi za Kiturkana ..... 42

2.2.1 Miundo ya silabi ya Kiturkana ..... 43

SURA YA TATU ..... 49

3.0 MABADILIKO YA KIFONOLOJIA YA KONSONANTI ZA NOMINO MKOPO ZA KITURKANA KUTOKA KISWAHILI ..... 49

3.1 Utangulizi ..... 49

3.2 Mifanyiko ya kimofofonolojia ya konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana ..... 51

3.2.1 Kudhoofika kwa konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana ..... 51

3.2.2 Kuimarika kwa konsonanti ..... 53

3 .2.3 Kudondoshwa kwa konsonanti ..... 55

3.2.4 Udondoshaji wa /m/ ........ 56

3.2.5 Udondoshaji wa /n/ ........ 57

3.2.6 Udondoshaji wa /h/ ........ 58

3.2.7 Udondoshaji wa /j/ ........ 59

3.2.8 Udondoshaji /w/ ........ 60

3.3 Uchopekaji wa konsonanti ........ 60

3.3.1 Uchopekaji wa /n/ ........ 61

3.4 Usilimisho pamwe wa nazali ........ 62

3.5 Ubadala wa konsonanti ........ 64

SURA YA NNE ........ 66

4.0 MABADILIKO YA KIFONOLOJIA YA VOKALI ZA NOMINO MKOPO ZA KITURKANA ........ 66

4.1 Udondoshaji wa vokali ........ 67

4.1.1 Udondoshaji wa vokali /i/ ........ 68

4.2 Uchopekaji wa vokali ........ 70

4.2.1 Uchopekaji wa vokali /a/ ........ 71

4.2.2 Uchopekaji wa vokali /ɛ/ ........ 72

4.2.3 Uchopekaji wa vokali /u/ ........ 73

4.2.4 Uchopekaji wa vokali /i/ ........ 74

4.3 Uyeyushaji ........ 75

4. 3. 1 Ubadala wa vokali ........ 78

4.3.2 Uwiano wa vokali ........ 81

SURA YA TANO ........ 84

5.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI .................................................. 84

5.1 Utangulizi .................................................................................................. 84

5.1.1 Vipengele vya fonolojia ya Kiturkana .................................................... 84

5.1.2 Mabadiliko ya kifonolojia ya konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana ............ 85

5.1.3 Mabadiliko ya kifonolojia ya vokali za nomino mkopo za Kiturkana .................... 85

5.2 Muhtasari wa utafiti ..................................................................................... 85

5.3 Mapendekezo ............................................................................................... 86

MAREJELEO ................................................................................................... 87

VIAMBATANISHO ............................................................................................ 93

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Utafiti wetu unahusu uchanganuzi wa kimofofonolojia wa nomino mkopo kutoka Kiswahili hadi Kiturkana. Utafiti huu unalenga kuweka bayana mifanyiko ya kimofofonolojia ambayo nomino mkopo kutoka Kiswahili hupitia zinapoingizwa katika Kiturkana. Ni bayana kwamba kila lugha hudhihirisha ukopaji wa kiwango fulani wa maneno kutoka lugha nyingine na kwamba maneno hayo mkopo hupitia mabadiliko ya kimofofonolojia yanapoingizwa katika lugha pokezi. Pia lugha mbili au zaidi zinapotagusana, ukopaji wa maneno huweza kutokea ambapo lugha ya hadhi ya chini hukopa kutoka kwa lugha ya hadhi ya juu. Utafiti wetu unajikita katika ukopaji wa hadhi kwani Kiswahili kina hadhi ya juu kuliko Kiturkana kwani ni lugha rasmi na lugha taifa kulingana na katiba ya Kenya iliyopitishwa mwaka 2010. Nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili zimepitia mabadiliko ya kimofofonolojia ndipo zikubalike katika Kiturkana.

Kulingana na Habwe, Matei na Nyonje (2010), Ukopaji ni hali ya lugha moja kuchukua vipengele vya lugha nyingine na kuviingiza katika mfumo wake na kwamba msamiati ndio kipengele kinachokopwa zaidi. Lugha hukopa msamiati ili kuelezea wazo jipya ambalo halikuwepo katika utamaduni wake. Kwa mfano Wataalamu kama vile Whiteley (1967), Lyons (1968), Bynon (1977), Mbaabu (1996) na Mwita( 2009), wanaeleza maneno mkopo kama uhamishaji wa leksia kutoka lugha moja hadi nyingine. Wataalamu hawa wanafikiana kwamba lugha hukopa leksia zozote lakini ni nomino ndizo hukopwa kwa wingi ili kuelezea dhana geni katika lugha pokezi. Tunaafikiana na wataalamu hawa

kwa sababu Kiturkana kimekopa nomino za Kiswahili ili kuelezea dhana ambazo hazikuwepo katika utamaduni wake.

Ukopaji ndiyo mbinu inayotumika sana katika uundaji wa maneno mengi katika lugha nyingi duniani. Ukopaji unaweza kuwa maneno, miundo ya sentensi na hata lafudhi. Utafiti wetu unajikita katika ukopaji wa nomino. Kuna aina mbalimbali za ukopaji kama vile: ukopaji wa tafsiri ambapo maana ya maneno hutafsiriwa kwa kujikita katika lugha changizi au chanzi. Kwa mfano neno la Kiingereza *armyworm* itakuwa viwavi jeshi katika Kiswahili. Utohozi ni njia nyingine ya ukopaji ambapo maneno mkopo huchukua maendelezo ya lugha pokezi. Kwa mfano *television* limetoholewa kuwa televisheni katika Kiswahili. Ukopaji sisisi ni kule lugha pokezi huyachukua maneno ya lugha changizi na kutumia vivyo hivyo bila kuyafanyia mabadiliko yoyote. Hatimaye kuna ukopaji wa vipengele vingine vya kiisimu ambapo lugha pokezi huweza kukopa vipengele vya kimofolojia na kimofosintaksia. Lugha pokezi huweza kukopa sauti ambazo haikuwa nazo awali kutoka lugha nyingine. Kwa mfano kuna tafiti ambazo zimeonyesha kwamba ukopaji huweza kuleta mabadiliko ya kifonolojia katika lugha pokezi. Kwa mfano, Newsmann (2000) anatoa mfano wa Kihausa ambacho hakikuwa na fonimu /h/ kabla ya kutagusana na lugha ya Kiarabu. Mwanzoni, sauti /h/ ilikuweko katika Kihausa lakini kama alofoni ya sauti /f/ ikitokea kabla ya vokali za nyuma. Kwa mfano, dafu [dahu] kutoka na athari ya lugha ya Kiarabu /h/ ikaanza kutumika katika lugha ya Kihausa.

Kulingana na Iribemwangi na Mukhwana (2010) ukopaji wa maneno huundwa sambamba na urekebishaji wa neno hili lifuate kanuni za kifonolojia za lugha pokezi. Kwa hivyo nomino zinazokopwa hupitia mabadiliko ili kukubadilika katika lugha pokezi. Wanatoa mfano wa lugha ya Kiswahili ambayo imejiongezea msamiati kwa mbinu ya ukopaji ambapo neno geni hupururwa, likatolewa ugeni ili liweze kuingiana na muundo wa maneno ya lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo hiyo lugha pokezi haiwezi kulemazwa na miundo mipya kutoka lugha changizi. Vile vile wanasema kwamba utohozi kama mkakati wa kukuzia lugha kimsamiati ungesaidia kuepusha mkanganyiko uwezao kutokea iwapo neno fulani linalotumika katika lugha ya kawaida lingepewa hadhi ya kuwa istilahi ili kuelezea dhana mpya. Aidha, wanaeleza kwamba baada ya neno kutoholewa, neno hilo hutolewa ule uasilia wake kiasi cha kulifanya lifuate mfumo wa lugha pokezi kifonolojia na kimofolojia. Kwa mfano neno kioski linahakikiwa kama neno la asili ya Kiswahili ndio maana watu huchukua kuwa wingi wa *kioski* ni *vioski.*

Wataalamu kama vile Whiteley (1967), Lyons (1968), Bynon (1977), Mbaabu (1996) na Mwita ( 2009), wanaeleza maneno mkopo kama uhamishaji wa leksia kutoka lugha moja hadi nyingine. Wataalamu hawa wanafikiana kwamba lugha hukopa leksia zozote lakini ni nomino ndizo hukopwa kwa wingi ili kuelezea dhana geni katika lugha pokezi. Tunakubaliana na wataalamu hawa kwani Kiturkana kimekopa nomino nyingi kutoka kwa Kiswahili kuliko kategoria nyingine za maneno.

### 1.0.1 Lugha ya Kiturkana

Kiturkana huzungumzwa na jamii ya Waturkana ambao wanaishi Kaskazini Magharibi mwa Kenya katika kaunti ya Turkana. Pia huzungumzwa katika kaunti ya Marsabit, Isiolo na eneo la Baragoi katika kaunti ya Samburu. Hata hivyo wazungumzaji wengi wazaliwa wa Kiturkana wanapatikana katika kaunti ya Turkana. Lugha hii imeenea katika mataifa jirani ya Ethiopia, Sudan na Uganda. Kulingana na Barrett (1990) Kiturkana ni kundi la lugha ya ambalo lina ukaribu na lugha ya Karamoja, Jie, jiye, Dodoth, Teso, Topasa na Nyangatom. Kiturkana kipo katika kundi la *ngitunga* yaani watu. Kwa mfano, Diana Lesley – Neuman katika makala yake, *Morphonological levels and grammaticalization in Karamojong,* anaeleza kwamba Kijie, kidoth, Kitoposa, Kinyangatom na Kiturkana zina asilimia themani na tano ambao upo katika Kiramojong.Aidha, Diana Lesley anawanukuu Novelli (1985) na Dimmendaal (1983) katika makala hayo *Morphonological levels and grammaticalization in Karamojong* ambao wanadai kwamba historia simulizi ya Waturkana na Wakaramojong inaonyesha kwamba walikuwa kikundi kimoja hapo awali.

Kiturkana ni lugha iliyo na vitenzi jina changamano, toni nyingi na njeo nyingi zinazowezesha wazungumzaji wazawa wa Kiturkana kuwasiliana na kueleza dhana mbalimbali. Naye Dimmendaal (1983) anaeleza kwamba Kiturkana ni mojawapo ya lugha ambazo utamkaji wa maneno mengi huegemea kiasi ya toni.

Kiturkana kimetagusana na Kiswahili kwa muda mrefu tangu wakoloni na wamishonari wa dhehebu ya Kikatoliki walipotuama katika kaunti ya Turkana wakati huo ikiwa wilaya

ya Turkana. Wakoloni na wamishonari walikuja na vitu ambavyo havikuwepo katika utamaduni wa Kiturkana. Pia wamishonari wa kanisa Katoliki walianzisha shule katika tarafa ya Lorugumu na walitumia Kiswahili kuwafunza wanafunzi kutoka Turkana. Aidha, waliofunzwa kazi za ufundi kama vile useremala, uashi na upishi walifunzwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo lugha iliyofahamika na Waafrika wengi, wakoloni na wameshonari hawakuwa na budi kutumia Kiswahili na kwa njia hiyo Kiturkana kikakopa nomino nyingi kutoka kwa Kiswahili.

Ingawa Kiturkana kimekopa nomino kutoka lugha nyingine kama vile kutoka Kipokot, Kikaramojok, Kijie, Kitoposa na Kimerile lakini za Kiswahili ndizo zimekopwa kwa wingi ili kuelezea dhana mbalimbali geni ambazo hazikuwepo katika utamaduni wake. Nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili zinapotamkwa zinatamkwa kwa kuzingatia mfumo wa lugha ya Kiturkana. Hii ina maana kwamba nomino zilizokopwa kutoka Kiswahili hupitia mabadiliko ya kimofofonolojia. Mabadiliko hayo ndiyo hayajawekwa wazi kwa kuelezwa kitaaluma. Hii ndio maana utafiti wetu umechukua dafina hii kuziba pengo hili muhimu ya kiisimu.

### 1.0.2 Lugha ya Kiswahili

Kiswahili ni mojawapo wa lugha ya kibantu kulingana na Guthrie (1971). Aidha , Milan G. P. de Lany (1967) anaunga kauli hii ya Guthrie kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu na kama lingua franka kimekopa maneno mengi kutoka lugha nyingine kama vile Kiarabu na Kiingereza. Pia anadai kwamba Kiswahili kina dhima ya kutumiwa katika maeneo ya mipakani na lugha ya mawasiliano miongoni wa watu wa lugha

mbalimbali. Aidha ni lugha yenye utamaduni, elimu na mawasiliano katika eneo kubwa ya Afrika.

Naye Bakari (1982) anasema kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika inayozungumzwa na watu wengi zaidi katika Afrika Mashariki na kati. Anaungwa mkono na Iribemwangi na Mukhwana ambao wametaja Kiswahili kama Lingua Franka inayozungumzwa na watu wengi katika maeneo ya Kusini mwa Sahara barani Afrika. Aidha, Massamba (1990)anaeleza kwamba Kiswahili ni lugha ya Kwanza kwa watu wanaoishi mwambao wa Afrika kuanzia Somalia upande wa kaskazini hadi visiwa vya komoro upande wa kusini.

Kiswahili vile vile kinatumika katika idhaa nyingi za Redio kama vile idhaa ya Kiswahili ya BBC, sauti ya Amerika, Redio China Kimataifa, Redio Terna na Redio Japan. Nchini Kenya Kiswahili kimepewa hadhi na katiba mpya ya (2010) kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi. Kiswahili kwa hivyo hutumiwa katika shughuli rasmi nchini Kenya mathalan katika asasi za elimu, mahakamani, sherehe rasmi za serikali na bungeni. Na kama lugha ya taifa Kiswahili kinatumiwa katika shughuli za kibiashara, usafiri na hata kuelezea sera za serikali mashinani.

## 1.1 Suala la utafiti

Tatizo la utafiti wetu limetokana na ukosefu wa kazi iliyoshughulikia uchanganuzi wa mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka lugha ya Kiswahili. Utafiti wetu unakusudia kuziba pengo hili.

Kwa muhtasari tumefupisha masuala tuliyodara kwa maswali yafuatayo:

i) Ni mabadiliko yapi ya sauti ambayo hutokea wakati nomino za Kiswahili zinaingizwa katika Kiturkana?

ii) Ni marekebisho gani ya sauti ambayo hutokea wakati nomino za Kiswahili zinakopwa na kuingizwa katika Kiturkana?

Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya na kinazidi kushamiri na kuenea kila kukicha katika pembe zote za taifa letu la Kenya. Mtagusano wa wazungumzaji wa Kiswahili na Kiturkana umekifanya Kiturkana kukopa nomino kutoka Kiswahili. Nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili zimepitia michakato fulani ya kimofofonolojia ili kuafiki mfumo wa Kiturkana. Waaidha, ni dhahiri shahiri kwamba mtu yeyote anaweza kuainisha nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Hata hivyo kuna haja ya kushughulikia tatizo hili kitaaluma, ndipo utafiti wetu utashughulikia tatizo hili kwa kutumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia (NFZA) ili kuweka bayana michakato ya kimofofonolojia zinazopitiwa na nomino mkopo kutoka Kiswahili hadi Kiturkana. Utafiti wetu kwa hivyo utaainisha nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili kifonetiki na kiothografia katika uchanganuzi wetu.

## 1.2 Malengo ya utafiti

Utafiti huu unaongozwa na malengo yafuatayo:

i) Kuchunguza vipengele vya fonolojia vya Kiturkana kama kama vile irabu, nusu-Irabu, konsonanti, na silabi

ii) Kubaini mabadiliko ya sauti yanayokumba konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

iii) Kutambua mabadiliko ya vokali yanayotokea katika nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili na mazingira ya mabadiliko hayo.

## 1.3 Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa kwa kuwa unahusu ukopaji wa nomino kutoka Kiswahili hadi Kiturkana. Hii ina maana kwamba utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa katika Isimu linganishi kwa sababu unahusu Kiswahili na Kiturkana.

Kulingana na uchunguzi tuliofanya maktabani na mtandaoni, utafiti huu ndio wa kwanza kufanywa kuhusiana na mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hivyo basi utakuwa mchango aali kwa taaluma ya isimu ya lugha za Kiafrika.

Utafiti huu pia utakuwa wa manufaa kwa wale ambao watataka kutafiti lugha ya Kiswahili kwa kulinganisha na lugha nyingine zisizo za kibantu. Isitoshe wanafunzi wa shule za msingi na upili wataweza kuboresha matamshi yao katika Kiswahili kwa kuepuka kutamka baadhi ya nomino za Kiswahili namna zinavyotamkwa katika

Kiturkana. Aidha, kazi hii itakuwa mchango katika taaluma ya tafsiri na uundaji wa kamusi ya Kiturkana –Kiswahili, na majarida mengine ambayo yanaweza kuwafaidi wazungumzaji wa Kiturkana na Kiswahili.

## 1.4 Nadharia tete

Utafiti wetu umejikita katika haipothesia zifuatazo:

i) Vipengele vya fonolojia ya Kiturkana kama vile fonimu na silabi vina uhusiano wa moja kwa moja na nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

ii) Konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hubadilika na kufuata ruwaza fulani.

iii) Vokali za nomino mkopo za Kiturkana hubadilika na kufuata mfumo na ruwaza fulani.

## 1.5 Upeo wa utafiti

Utafiti wetu utashughulikia ukopaji wa nomino kutoka Kiswahili hadi Kiturkana kwa kuzingatia mifanyiko ya kimofofonolojia. Kiturkana kimekopa maneno kutoka lugha nyingine kama vile Kiingereza, Kipokot, Kirendile, Kimerile na Kiramojok. Utafiti huu hautashugulikia nomino mkopo kutoka nyingine bali utajikita tu katika nomino mkopo kutoka Kiswahili.

Aidha, tutatumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia katika uchanganuzi wetu.

Katika kuchunguza mabadiliko ya kimofofonolojia hatutadara elementi kama vile toni, mkazo na kiimbo za nomino mkopo za Kiturkana.

Kwa sababu mtafiti ana umilisi wa Kiturkana na Kiswahili, tumechota data yetu maktabani yaani kutoka kwa Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili, misali ya Kiturkana na Bibilia ya Kiturkana.

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Utafiti wetu ulitalii machapisho mbalimbali kuhusu ukopaji na mifanyiko ya kimofofonolojia ili kutupa mwanga zaidi kuhusu utafiti huu. Maandishi tuliyorejelea katika utafiti wetu ni ya kijumla na yale bayana kuhusu ukopaji wa maneno.:

### 1.6.1 Maandishi ya Kijumla kuhusu ukopaji wa maneno

Wataalamu kama vile Mbaabu (1966), Whiteley ( 1967), Lyons (1968), Bynon (1977) na Mwita (2009) wameeleza maneno mkopo kama uhamishaji wa leksia kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa hivyo wataalamu hawa wanaafikiana kwamba lugha huweza kukopa leksia lakini nomino ndizo hukopwa kwa wingi. Kazi hizi zina manufaa kwetu kwani kazi yetu inashughulikia nomino mkopo za Kiswahili katika Kiturkana. Hata hivyo kazi hizi hazituelezi kuhusu michakato ya kimofofonolojia ambayo nomino zinazokopwa kutoka lugha nyingine hupitia ndipo zikukubalike katika mfumo wa lugha pokezi. Kwa sababu hii kazi yetu itadhihirisha mifanyiko ya kimofofonolojia ambayo nomino zinazokopwa kutoka Kiswahili hadi Kiturkana hupitia ndipo zikubalike katika mfumo wa Kiturkana.

Kazi nyingine tuliyorejelea ni Poplack (1988) anayedai kwamba nomino ndio kategoria ya maneno ambayo yanapatika katika ukopaji zaidi ya maneno mengine kwa kuwa

nomino ndio hubeba maudhui katika lugha. Kazi hii ina ukuruba na kazi yetu kwani tunashughulikia nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Hata hivyo kazi hii haionyeshi mifanyiko ya kifonolojia ambayo nomino mkopo hupitia ndipo zikubalike katika lugha pokezi. Kwa hivyo kazi yetu itaweka bayana mifanyiko ya kimofofonolojia ambayo nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hupitia.

Field (2002) anayesema kwamba nomino zina uwazi wa maana na kwa sababu hii nomino hukopwa zaidi kuliko maneno mengine. Kauli ya kazi hii kwamba nomino zina uwazi wa maana hivi kwamba ndizo zinazokopwa zaidi ina ukweli kwani nomino hutaja kitu, mtu, dhana au cheo. Kwa sababu hii nomino mkopo za Kiswahili katika Kiturkana zina maana bayana. Hata hivyo kazi hii haituelezi kwa kina ni maana gani.

Moravesiks (1978) anasema kwamba ukopaji wa nomino ni jambo la kawaida wakati lugha zinapotagusana na lugha hizi husika huendelea kukopa kategoria nyingine za maneno ilmuradi nomino ndizo zimekopwa mwanzo. Tunakubaliana na kauli ya kazi kwani Kiturkana kimekopa kwanza nomino za Kiswahili baada ya mtagusano kati ya Kiturkana na Kiswahili ili kutajia dhana na vitu visivyo katika utamaduni wa wasemaji wa Kiturkana. Ufinyu wa kazi hii ni kwamba hajashughulikia mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo katika lugha husika.

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanaeleza ukopaji kama mbinu inayotumika sana katika uundaji wa maneno mengi katika lugha nyingi duniani na kwamba maneno yanayokopwa huenda sambamba na urekebishaji ili yafuate kanuni za kifonolojia za

lugha pokezi. Wanatoa mfano wa maneno mkopo katika lugha ya Kiswahili ambayo yalitoholewa kwanza kisha yakafanywa yafuate mfumo wa Kiswahili kifonolojia na kimofolojia hivi kwamba watu wengi kuhakikiwa kama maneno yenye asili ya Kiswahili. Tunakubaliana na kauli ya Kazi hii kwamba maneno yanayokopwa hurekebishwa ili yafuate mfumo wa kifonolojia na mofolojia ya lugha pokezi. Hata hivyo kazi hii inataja tu kwamba maneno mkopo hurekebishwa ili yakubalike katika mfumo wa lugha pokezi bila kutueleza kuhusu bayana mabadiliko ya kifonolojia yanayokumba maneno mkopo hayo.

Aidha, Hockett (1958) na Weinreich ( 1963) kwamba lugha inayokopa huwa haipotezi chochote wakati inakopa neno na kwamba istilahi ya ukopaji huenda sambamba na masharti ya lugha chanzi. Kauli hii ni sawa kwani Kiturkana kimekopa kutoka Kiswahili na nomino mkopo zilizokopwa zimepitia michakato ya kifonolojia. Kwa upande mwingine kazi hii ya Hockett na Weinreich haituelezi kwa kina kuhusu masharti ambayo maneno mkopo yanafaa kuafiki ndipo yakubalike katika mfumo wa lugha pokezi.

Nao Habwe, Matei na Nyonje (2010) wanaeleza ukopaji wa lugha kama hali ya lugha kuchukua vipengele vya lugha nyingine na kuviingiza katika mfumo wake. Vipengele ambavyo vya lugha vinakopwa ni msamiati. Wanatueleza kwamba lugha changizi huwa na hadhi ya juu ikilinganishwa na lugha pokezi. Wataalamu hawa wanadai kwamba ukopaji unaweza kuwa ukopaji tafsiri, utohozi , ukopaji sisisi na ukopaji wa vipengele vya kiisimu. Maelezo ya watafiti hawa yametufaa pale ambapo wanatupa mifano ya maneno yaliyotoholewa katika lugha ya Kiswahili yanavyobadilika na kufuata mfumo wa

kifonolojia kwa mfano: *Baiskeli* kutoka neno la Kiingereza. Maelezo yametusaidia kuweza kutambua nomino mkopo za Kiturkana kutoka lugha ya Kiswahili. Waaidha, maelezo yao kuhusu vipengele vya kimofolojia na kimofosintaksia ambapo wanatoa mfano maneno mkopo ya Kiswahili kutoka Kiarabu ambayo yana sauti /kh/ na /gh/. Ufinyu wa kazi hii ni kwamba hajashughulikia kwa mapana na marefu vipengele vya fonolojia ya nomino mkopo.

Newman (2000) anayesema kwamba Kihausa hapo awali hakikuwa na fonimu /h/ kabla ya mtagusano wake na Kiarabu. Kazi pia itatusaidia kutambua mabadiliko ya sauti ambayo nomino za Kiswahili hupitia yanapoingizwa katika lugha ya Kiturkana. Hata hivyo maelezo ya kazi hii haijabainisha mabadiliko ya kimofofonolojia ambayo maneno mkopo ya Kiswahili hupitia. Aidha hawajatumia nadharia yoyote kueleza mabadiliko ya kimofofonolojia ambayo maneno mkopo hayo hupitia.

### 1.6.2 Maandishi bayana kuhusu ukopaji

Njuguna (1992) katika tasnifu yake ya uzamili ameshughulikia mofofonolojia ya Kiswahili na Kikuyu sanifu ambapo amelinganisha mofofonolojia za Kiswahili sanifu na lahaja za Kikuyu. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti wetu kwa vile imeshughulikia mofofonolojia ya Kiswahili na nadharia inayotumiwa ni ya fonolojia zalishi asilia tunayotumia katika uchunguzi wetu. Hata hivyo, kazi ya Njunguna ina maelezo mafupi sana hususan katika kuelezea sheria ya nadharia ya fonolojia zalishi kwa mfano hajashughulikia ukaakaishaji. Aidha, analinganisha mofofonolojia ya Kiswahili sanifu na

Kikuyu sanifu, lakini kazi yetu haishughulikii ulinganishaji bali inayoshughulikia michakato ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

Kazi nyingine ambayo tumerejelea katika utafiti wetu ni ya Iribemwangi (2008) ambapo anatoa maelezo kuhusu ukopaji katika lugha ya Kiswahili kutoka lugha kama vile Kiingereza, Kiarabu, Kiajemi na Kireno. Maneno mkopo hayo yanatoholewa kupitia michakato kama vile ubadilishaji, uchopekaji na udhoofishaji wa konsonanti na vokali. Mchakato huu wa kifonolojia unayafanya maneno mkopo kukubalika kileksika katika Kiswahili sanifu. Kazi hii ya Iribemwangi ina manufaa kwetu kwani imeshughulikia mabadiliko ya kimofofonolojia nomino mkopo katika lugha ya Kiswahili. Isitoshe, ametumia nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia (NFZA) ambayo utafiti wetu utatumia. Hata hivyo, kazi hii ya Iribemwangi imeshughulikia maneno mkopo katika lugha sanifu ya Kiswahili huku utafiti wetu ukishughulikia nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

Bakari (1982) amelinganisha na kutofautisha mofofonolojia ya lahaja mbalimbali za Kiswahili. Kazi hii ni muhimu kwa kazi yetu kwani imetupa mwanga kuhusu mofofonolojia. Tofauti iliyopo kati ya kazi hii na yetu ni kwamba kazi yetu inahusu mofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

Maringah (1987) ameshughulikia mabadiliko ya sauti katika matamshi ya Kimbeere na Kiswahili. Kazi hii inadhihirisha michakato ya kifonolojia kwa kutumia nadharia ya Joan Hooper ya fonolojia zalishi asilia. Kazi hii ya Maringah japo ina uhusiano na kazi

yetu, ni fupi kwani haijaeleza kwa kina mabadiliko yote ya kimofofonolojia. Kwa hivyo, utafiti wetu utaeleza michakato yote ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana. Waaidha kazi hii ya Maringah imeshughulikia Kimbeere ilhali kazi yetu inashughulikia Kiturkana.

Ngowa (2015) ameshughulikia mofofonolojia ya nomino mkopo zinazohusu vifaa vya pikipiki kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kigiriama. Kazi hii ina umuhimu kwetu kwani inahusu mofofonolojia na inatumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia sawa na kazi yetu. Tofauti iliyopo ni kwamba kazi ya Ngowa imejikita katika nomino mkopo za vifaa vya pikipiki katika Kigiriama kutoka Kiingereza lakini utafiti wetu unajikita katika nomino mkopo za Kiturkana kutoka lugha ya Kiswahili. Kazi nyingine iliyo na ukuruba na Ngowa ni ya Evans (2014) ambapo ameshughulikia mabadiliko ya maneno mkopo ya Kiingereza katika Kibukusu ambapo ametumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia. Udhaifu wa kazi hii ya Evans hajaieleza kwa kina namna sheria za nadharia ya fonolojia zalishi asilia inaeleza kuhusu mabadiliko ambayo nomino mkopo za Kiingereza hupitia zinapoingia katika Kibukusu.

Mwihaki (1998) ameshughulikia kanuni za fonolojia ambazo zinaelekeza maneno yanayokopwa kutoka Kiingereza hadi lugha ya Kikuyu. Utafiti wake unatupa sababu zinazofanya lugha ya Kikuyu kukopa kutoka Kiingereza. Utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu japo ametumia nadharia ya fonolojia zalishi ambayo ni tofauti na nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Tofauti nyingine na utafiti

wetu ni kwamba Mwihaki anashughulikia maneno mkopo kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kikuyu na yetu inahusu nomino mkopo kutoka Kiswahili hadi Kiturkana.

Mberia (1993) ameshughulikia ya mofofonolojia ya Kitharaka kwa kutumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia. Amechunguza mabadiliko ya konsonanti na vokali katika Kitharaka kwa kueleza sheria zinazohusika, vile vile kazi hii imechunguza msamiati mkopo kutoka Kiswahili hadi Kitharaka. Kazi hii imetufaa katika utafiti japo kazi yetu inashughulikia mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

Barton (1921) katika makala yake ya *Turkana Grammatical Notes and vocabulary* anadai kwamba ni Waturkana wachache ambao huzungumza Kiswahili na Kuzungumza Kisuk kiasi fulani. Kazi imetupa mwanga kwamba Kiswahili kimetagusana na Kiturkana kwa muda mrefu hivi kwamba kukopa kutoka Kiswahili. Hata hivyo kazi hii hajashughulikia mabadiliko ya kifonolojia za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili ambayo kazi hii yetu inashughulikia.

Mwaliwa (2000) katika tasnifu yake ya uzamili;Ulinganishi wa Mofofonolojia ya Kiswahili na Kidawida ambapo amelinganisha mofofonolojia ya Kiswahili sanifu na Kidawida ni marejeleo muhimu katika kazi hii kwani kazi yetu pia inahusu mofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Hata hivyo Mwaliwa ameshughulikia ulinganishi wa mofofonolojia ya Kiswahili na Kidawida ilhali kazi yetu inahusu mofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

Mulwa (2014) ameshughulikia mofofonolojia ya nomino mkopo za Kikamba kutoka Kiswahili. Kazi ya Mulwa ina manufaa kwetu kwani inahusu mabadiliko ya mofofonolojia. Hata hivyo Mulwa ametumia nadhari ya fonolojia vipande sauti tofauti na yetu ambayo ni fonolojia zalishi asilia. Aidha kazi yake Mulwa inashughulikia nomino mkopo za Kikamba ilhali kazi yetu inashughulikia nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

Kadege na Mabungu (2009) wamedara ukopaji wa maneno kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kishona ambapo wanaonyesha kwamba wazungumzaji asilia wa lugha ya Kishona wanategemea michakato ya kifonolojia ikiwemo ya vipande-sauti, uchopekaji, na uundaji wa upya wa maneno mkopo ili yaweze kuafiki muundo wa fonolojia ya lugha ya Kishona. Kazi hii itatufaa kwani imetupa mwangaza kuhusu mifanyiko ya kimofofonolojia kama uchopekaji. Hata hivyo nadharia ambayo imetumiwa na wataalamu hawa ni tofauti ya yetu.

Kembo-Sure (1993) anaeleza jinsi maneno mkopo kutoka Kiingereza hadi Kidholuo yanavyozingatia vigezo vya kisarufi na kifonolojia. Kembo anaendelea kutuelezea kuhusu vipande sauti katika sifa arudhi katika maneno mkopo kutoka kiingereza hadi Kidholuo. Waaidha , Kembo-Sure (1993) anasema kwamba ukopaji ni mmojawapo ya michakato ya kihalisia ambapo huhusisha utohozi wa maneno mageni kwa kuyabadilisha ili yapate kukubalika katika lugha inayokopa. Mchango wa huu wa Kembo-Sure utatufaa katika utafiti wetu kwani unadara mageuzi ya kifonolojia ya vipande sauti vya maneno mkopo na nadharia aliyotumia ya Fonolojia Zalishi Asili ndio

tutakaotumia katika utafiti wetu. Tofauti ni kwamba kazi ya Kembo inashughulikia Kidhuluo ilhali kazi yetu inashughulikia Kiturkana.

Naye Hyman (1970) anasema kuwa jukumu la ukopaji katika sarufi ni kwamba sauti hukopwa ili kupima matamshi ya maneno yanayokopwa. Hyman anasisitiza kwamba lugha hufuata sauti za lugha kopaji ziznazokaribiana na zile za lugha kopeshi. Hyman anahusisha maneno mkopo kutoka lugha ya Kihispaniola. Mawazo haya ya Hyman yatatusaidia katika utafiti wetu kwani yanadara vikwazo vya kifonolojia vinavyopitiwa na sauti za lugha ya Kihakui zinapokopwa hadi lugha ya Kihispaniola.

Kulingana na Katamba na Rottland (1987) wameshughulikia ukopaji wa silabi za Kiingereza katika lugha ya Luganda na kuonyesha kuwa konsonanti za vianzio vya maneno ya Kiluganda zinawekewa mipaka kuliko zile za Kiingereza kwa hivyo katika ukopaji silabi ni kama kichungi cha kuchungia maneno mkopo yanayoingizwa katika Kiluganda. Makala haya ya Katamba na Rottland (1987) yatatufaa katika utafiti kwa kuwa yanadara mabadiliko ya muundo nje katika ukopaji wa maneno. Aidha,yanaonyesha kwamba fonolojia ina jukumu la kipekee katika mchakato wa ukopaji wa maneno. Hata hivyo tofauti na utafiti wetu ni kwamba Katamba na Rottlanda wameshughulikia lugha ya Luganda na Kiingereza ilhali utafiti wetu unahusu ukopaji wa nomino kutoka Kiiswahili hadi Kiturkana.

Habwe na Karanja (2004) wameeleza mabadiliko ya kimofofonolojia katika lugha ya Kiswahili na kutoa mabadiliko ambayo konsonanti na vokali hupitia. Kazi yao

imetusaidia kuelewa mabadiliko ya kimofofonolojia katika Kiswahili. Hata hivyo kazi hii yao hajaeleza mabadiliko ya kimofofonolojia kwa kutumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia ili kuweka wazi mabadiliko hayo.

Mgullu (1999) ameshughulikia fonolojia ya Kiswahili sanifu kwa kujikita kwa nadharia ya Fonolojia Zalishi. Hata hivyo Mgullu ameshughulikia mofofonolojia kama kijimada tu bila kufafanua mifanyiko ya kimofofonolojia kwa kina. Tofauti nyingine kati ya kazi ya Mgullu na kazi yetu ni kwamba Mgullu ameshughulikia fonolojia ya Kiswahili pekee ilhali utafiti wetu unashughulikia fonolojia ya Kiturkana na mifanyiko ya kimofofonolojia nomino mkopo za Kiturkana.

Kazi nyingine ambayo tumerejelea katika kazi yetu ni Hyman (1975) ambaye ameshughulikia kwa kina na uketo fonolojia zalishi, ambapo amejadili kwa kina dhana ya mifanyiko ya kifonolojia na kanuni zake. Aidha ameeleza uhusiano kati ya fonetiki na fonolojia. Kwa wakati huo huo Hyman ameeleza sifa bainifu za fonimu ambazo ni muhimu katika uchanganuzi wowote wa kifonolojia. Kazi hii ya Hyman imetufaa katika kazi yetu kwani imetuwezesha kufahamu kanuni za Schane ambazo ni mojawapo za kanuni ya nadharia ya fonolojia zalishi asilia ambayo tunatumia katika kazi yetu.

Makala ya Diane lesley- Neuman (2012), *Morphonological levels and grammaticalization in Karamojong.* Yametufaa katika kazi yetu kwani mofofonolojia ya Kikaramojong kina uhusiano mkubwa na Kiturkana hususan kwa upande wa fonimu. Hata hivyo kazi hii ya Diane lesley-Neuman haijaeleza mifanyiko ya kimofofonolojia

kwa mapana na marefu na pia haijatumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia tunayotumia sisi katika kazi yetu. Isitoshe , kazi yetu inashughulikia michakato ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili tofauti na kazi ya Diane.

## 1.7 Msingi wa nadharia

Nadharia ambayo tumeteua kuelekeza utafiti wetu ni nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia (NFZA). Nadharia hii ilizuka ili kutatua udhaifu wa nadharia ya Fonolojia Zalishi ( FZ) uliodhihirika katika kazi za Noam Chomsky za miaka ya 1950. Kulingana na Sommerstein (1977) SPE ni kazi bora na hakuna nadharia za awali zimepiku SPE. Hata hivyo kauli hii ya mtalaamu huyu ni suala la mjadala.

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia imekuwa muhimu mno katika kutatua matatizo mawili ya Fonolojia Zalishi yaani tatizo la uundaji sheria au kanuni na udhahania.

Nadharia hii ya NFZA iliendelezwa na wasomi kama Vennemann (1972, 1974), Hooper (1975, 1976, 1979), Hudson (1975), Hyman (1975) na Rudes (1976). Hata hivyo Hooper ndiye aliyefafanua nadharia hii mwaka wa 1975 kwa kueleza kwamba NFZA inazingatia fonolojia huku ikitambua umuhimu wa mofolojia. Isitoshe, Hooper anapendekeza kwamba umuhimu mkubwa wa NFZA ni uwezo wake wa kuleta pamoja fonolojia na mofolojia ya lugha husika.NFZA inachunguza maumbo ya maneno ili kuondoa udhahania kwa kuonyesha muundo ndani ili kupata kukubalika kama muundo nje. . Hii ina maana kwamba humwezesha mchunguzi wa lugha husika kufikia utabiri halisi kuhusu lugha asilia. Nadharia hii kwa hivyo ina umuhimu mkubwa katika utafiti wetu. Joab Hooper anaita kauli hii kanuni ya ujumlishaji sahihi. Kanuni ya ujumlishaji

inawasilisha uhusiano kati ya maumbo nje na kauli za jumla ambazo lazima zidhihirishwe kama ya kweli katika neno husika. Hooper anasema kwamba kanuni ya ujumlishaji sahihi inaeleza kuwa sheria zinazowekwa na wazungumzaji wa lugha husika hutokana na maumbo nje ya maneno bali si maumbo ndani (1976) . Kanuni hii hairuhusu kurejelea kuwepo kwa sheria inayorejelea sehemu isiyokuwepo. Kwa hivyo sheria inadhibiti matumizi ya 'uwezekano' yaani udhahania. Vennemann anadai kwamba sheria za Fonolojia Zalishi zinaweza kutokea mara moja katika maneno bila kulazimishwa kwa mfuatano wa elementi au arki zinazohusika. Vennemann anasema kwamba sheria zote zinafuata ruwaza mahususi katika umbo lolote linalokubaliana na muundo wa maumbo. Kanuni ya ujumlishaji sahihi itasaidia kazi yetu kwa navyo maumbo huweza kudhihirishwa kifonetiki na kuyafanya kuwa na mantiki. Waaidha, kanuni hii itatusaidia kubaini kanuni ambazo zipo katika Kiturkana zinazodhibiti ukopaji wa nomino.

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia inajaribu kuondoa udhahania kwa kuonyesha kwamba muundo wa ndani uwe na uhusiano wa moja kwa moja na muundo nje. Hii ni kanuni ya uasilia kamili. Kanuni hii inasisitiza kwamba vipashio vya kifonolojia ambavyo vinajitokeza katika uwasilishaji wa kileska wa mofimu ni zile ambazo zinajitokeza katika muundo nje wa mofimu hiyo husika. kanuni hii ya uasilia halisi ni muhimu katika utafiti wetu kwani itatusaidia kuondoa udhahania kwa kuweka wazi maumbo ndani na maumbo nje ya nomino mkopo za Kiturkana.NFZA inagawa kanuni hizi kwa makundi manne:

### 1.7.1 Kanuni za kifonetiki

Kanuni hizi zinahusu michakato zilizo na habari za kifonetiki pekee. Hii ina maana kwamba kanuni hizi zinamotishwa kifonetiki . Kanuni hii huitwa kanuni za '**P**' Kanuni hizi ni zalishi na haziwezi kuzuiliwa. Kanuni '**P**' hufanya kazi katika maneno mkopo kutoka lugha ngeni. Waaidha kanuni hizi hufanya kazi katika mipaka ya silabi na mwisho wa neno peke. Kanuni hizi ni bia na hupatika katika lugha nyingi za ulimwengu. Kanuni za **'P'** hutumiwa kufafanua mabadiliko ya sauti kama vile udhoofikaji, uimarikaji, na usilimisho pamwe wa nazali. Kanuni hizi zimetusaidia kueleza mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati nomino za Kiswahili zinaingizwa katika Kiturkana.

### 1.7.2 Kanuni za mofolojia

Kanuni hizi zinahusu miundo za maneno katika mazingira ya mofosintaksia na leksia. Hii ina maana kwamba kanuni hizi huhusisha kanuni za kifonolojia katika mazingira ya kimofolojia au kisintaksia katika kategoria ya maneno kama vile wingi na njeo katika nomino, vitenzi, vielezi, vivumishi au viwakilishi. Kanuni hizi huhusu lugha fulani mahususi. Kanuni hizi huhusu maana katika lugha husika. Kwa mfano kuna mofimu inaonyesha hali wingi au njeo. Katika Kiturkana kwa mfano kuna mofimu inaonyesha jinsia kwa kuwa nomino ya Kiturkana hugawika katika jinsia ya kiume au kike. Kanuni hizi za mofolojia zimesaidia katika kazi hii yetu kwani imetuwezesha kutambua maumbo ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili baada ya kupitia mabadiliko ya kifonolojia kama vile uchopekaji wa vokali mwanzoni mwa nomino ili kubainisha jinsia ya nomino mkopo hiyo husika katika Kiturkana.

### 1.7.3 Kanuni za via

Kanuni hizi zinazoonyesha uhusiano maalum baina ya leksia za vipengele. Kanuni za Via huwezesha watu kuhusisha elementi au arki za kilesika ambazo hutofautiana kwenye miundo nje. Kulingana na Katamba (1989) kanuni za Via si zalishi na vipengele vichache vinavyohusishwa na kanuni za Via ni lazima ziwekiwa maki kibinafsi. Aidha, anaeleza kwamba kanuni fulani ya Via haiwezi kuchukuliwa kama umilisi wa mzawa lugha husika. Kanuni hizi za Via zitatufaa katika utafti wetu kutambua mabadiliko sauti yanayojiri katika nomino mkopo za kiturkana lakini maana ya kilesika kuhifadhiwa katika maumbo ya nomino mkopo hizi.

### 1.7.4 Kanuni za Sandhi

Kanuni hizi zinatokea kati ya kanuni za kifonetiki na kanuni za kimofolojia. Kanuni hizi huchukua mipaka za maneno. Wakati mwingine mpaka wa neno hufafana na mpaka wa kifonolojia hususan pale ambapo mpaka wa neno hufanana na mpaka wa silabi yaani mwanzo au mwisho wa silabi. Mipaka hiyo ikitokea hivyo, basi hutokea kama sheria za kifonetiki. Kanuni hizi zimetusaidia katika utafiti wetu kubainisha namna nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hubadilika ndipo zikubalike katika leksia ya Kiturkana. Aidha imetupa mwanga kuhusu mipaka ya silabi zinazodhihirishwa na Kiturkana hivi kwamba kutuwezesha kufahamu mabadiliko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili kwani baadhi ya mifanyiko hii inakusudiwa kupata silabi mwafaka ya nomino za Kiturkana. Aidha kanuni hii imetuwezesha kufahamu miundo ya silabi za Kiturkana na za Kiswahili.

## 1.8 Mbinu za utafiti

Ili kufikia malengo ya utafiti wetu kwa njia bora, tulijikita kwanza maktabani kutalii na kudurusu kazi mbalimbali zilizohusiana na utafiti wetu ili kupata mwelekeo mwafaka kuhusu mada na nadharia ya kutumia. Baada ya kudurusu machapisho mbalimbali maktabani yanayohusiana na mada ya kazi yetu, tulijikita maktabani kutalii data yetu yaani nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili katika kamusi ya Kiingereza — Kiturkana, misali ya Kiturkana na Bibilia ya Kiturkana. Tuliona ni vyema kuchota data yetu maktabani ili kuokoa muda na rasmali kwani ndiyo data ambayo tukipata tena nyanjani.

### 1.8.1 Uteuzi wa sampuli

Tuliteua nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili kutoka kamusi ya Kiingereza – Kiturkana, misali ya Kiturkana na Biblia ya Kiturkana. Nomino mkopo za Kiturkana tulizoteua ni kutoka Kiswahili wala si ya lugha nyingine kama vile Kiingereza, Kipokot, Kijie, Kisamburu, Kimerile au Ki. Hata hivyo hatujajishughulisha iwapo Kiswahili kilikopa nomino hizo mkopo. Japo mno mkopo ni nomino za Kiswahili ambazo Kiturkana kimezikopoa. Nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hizo tumeziambatanisha katika sehemu mwisho ya na mwisho ambapo tumeziandika kwa kifonetiki na kiothografia. Kwa kuwa mtafiti wa kazi hii ana umilisiKiswahili na Kiturkana ilikuwa rahisi sana kwake kutambua nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hivyo basi kupata sampuli tosha za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

### 1.8.2 Mbinu za kukusanya data

Mtafiti alikusanya data yake maktabani yaani kutoka kwa Bibilia ya Kiturkana, Misali na Kamusi ya Kiturkana- Kiingereza . Mtafiti alihakikisha kwamba data aliyokusanya maktabani ni nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili. Na kwa kuwa mtafiti ni mzawa mzungumzaji wa Kiturkana na aliye na umilisi wa Kiswahili ikawa rahisi kwake kutambua nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili.

### 1.8.3 Uchanganuzi wa data

Baada ya kudondoa na kunakili nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili maktabani, tulizinukuu kwa kutumia alama za kifonetiki ili kudhihirisha sauti za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili kwa madhumuni ya kutambua mabadiliko ya sauti yanayojiri wakati nomino za Kiswahili zinakopwa na Kiturkana. Tulibainisha sauti za nomino za Kiswahili na za nomino za Kiturkana. Baada ya kubainisha sauti za nomino za Kiswahili na za Kiturkana , tulionyesha mabadiliko ya sauti za nomino za Kiswahili hadi Kiturkana kwa kudhihirisha mabadiliko ya sauti hizo. Tulielekezwa na kanuni nne za nadharia ya fonolojia zalishi asilia kuthibitisha na kudhihirisha mabadiliko ya sauti ya nomino za Kiswahili hadi Kiturkana yaani mabadiliko ya kimofofonolojia. Aidha, tulibainisha kanuni za kifonolojia zinazoelekeza ukopaji wa nomino za Kiswahili hadi Kiturkana. Hatimaye tulitoa maelezo kuhusu mbadiliko ya sauti yaliyojiri na mazingira ambamo mabadiliko ya sauti hutokea kwa michoro mahususi.

### 1.8.4 Uwasilishaji wa data

Matokeo ya utafiti wetu yamewasilishwa kwa maelezo na udhihirishaji wa kanuni iliyotumiwa kuelezea mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Maelezo haya yamefafanua mabadiliko ya kimofofonolojia kama vile uchopekaji, udhoofikaji, uimarikaji, udondoshaji na usilimisho wa konsonanti na vokali za nomino mkopo za Kiturkana. Aidha, tumetumia majedwali na michoro kuwasilisha matokeo yetu.

SURA YA PILI

# 2.0 FONOLOJIA YA KITURKANA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunakusudia kubainisha fonimu zote za Kiturkana kwa kuzipambanua kwani fonimu hizi ndizo msingi wa utafiti wetu. Fonimu hizi za Kiturkana ndizo zitakazotusaidia kufahamu michakato ya kifonolojia inayojiri katika Kiturkana. Kwanza kabisa, tutabainisha fonimu za Kiturkana kwa kuzingatia namna zinavyotamkwa na mahali pa kutamkia. Pia katika sura hii tutashughulikia silabi za Kiturkana kwani utafiti huu unahusu uchanganuzi wa mofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili. Inatujuzu kujadili miundo ya silabi ya Kiturkana kwa sababu miundo ya silabi haiwezi kamwe kupuuzwa kwa kuwa mabadiliko ya sauti hutokea wakati fonimu zinatokea katika mazingira jirani. Aghalabu fonimu zilizo katika mazingira jirani huishia kuunda silabi.

### 2.1.1 Fonimu za Kiturkana

Wataalamu wachache sana wameshughulikia fonimu za Kiturkana tukilinganisha za Kiswahili. Kwa mfano Barret (1990) amegawa fonimu za Kiturkana kwenye makundi matatu yaani Konsonanti, irabu na nusu –irabu bila kuelezea namna zinatamkwa na mahali pa kutamkia. Naye Dimmendaal (1983) amezigawa fonimu za Kiturkana katika makundi mawili makuu yaani konsonanti na irabu. Aidha, Leiden (1983) ameshughulikia fonimu za Kiturkana kwa kuzianisha katika makundi matatu yaani konsonanti, viyeyusho na irabu. Hata hivyo wataalamu hawa hawajashughulikia kwa mapana na

marefu fonimu za Kiturkana. Kwa sababu hii utafiti wetu utashughulikia fonimu za Kiturkana kwa kina na uketo.

### 2.1.2 Fonimu za irabu za Kiturkana

Irabu ni fonimu ambazo hutamkwa kwa urahisi kwani hutamkwa bila hewa kuzuiliwa na ala za kutamkia. Katika fonetiki fonimu huainishwa kama refu au fupi, hata hivyo katika fonolojia vokali refu huchanganuliwa kama mfuatano wa irabu mbili kama tutakavyoona katika kazi hii.

Barret (1990) anadai kwamba Kiturkana kina konsonanti kumi na nane. Wazo hili la Barret kwamba Kiturkana kina irabu kumi na nane lilitokana na uchanganuzi awali wa Dimmendaal (1983) kwamba Kiturkana na irabu kumi na na nane. Leiden (1983) anaeleza kwamba Kiturkana kina irabu kumi na nane kama anavyoainisha kwenye jedwali lifuatalo:

| IRABU | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | i | ɪ | e | ɛ | a | ɔ | o | ʊ | u | i̥ | ɪ̥ | e̥ | ɛ̥ | ḁ | ɔ̥ | o̥ | ʊ̥ | u̥ |
| Juu | + | + | - | - | - | - | - | + | + | + | + | - | - | - | - | - | + | + |
| Chini | - | - | - | - | + | - | - | - | - | - | - | - | - | + | - | - | - | - |
| Nyuma | - | - | - | - | + | + | + | + | + | - | - | - | - | + | + | + | + | + |
| Ghuna | + | + | + | + | + | + | + | + | + | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Kaze | + | - | + | - | - | - | + | - | + | + | - | + | - | - | - | + | - | + |

Imenukuliwa kutoka Leiden ( 1983: 17)

Hata hivyo Dimmeendaal (1993: 131) anadai kwamba Kiturkana kina irabu tisa za msingi na zile zingine tisa ni hafifu. Uchunguzi wetu unakubaliana na Dimmendaal (1993:131) kwamba kuna irabu tisa za msingi katika Kiturkana kama ifuatavyo:

Kielelezo 2.0 : Irabu za Kiturkana

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| i | | | | u |
| | ɪ | | ʊ | |
| e | | | | o |
| | ɛ | | ɔ | |
| | | a | | |

Imenukuliwa kutoka Dimmendaal ( 1993: 131)

Irabu zote katika Kiturkana huweza kuwa [+ghuna] au [-ghuna]. Katika kiwango cha fonetiki irabu fupi na refu hutokea, hata hivyo katika fonolojia irabu fupi na refu huchanganuliwa kama mfuatano wa irabu mbili. Katika mipaka ya neno katika Kiturkana, uwiano wa irabu kuhusiana na sehemu ya juu au ya chini ya ulimi hutokea. Leiden (1983) anadai kwamba uwiano wa irabu katika mfumo katika mfumo wa uwiano irabu, irabu katika neno huwa katika seti ya kategoria moja, ambazo hubainishwa kwa mwinuko wa chini wa ulimi. Hata hivyo katika Kiturkana hali hii ina utata kutokana uwepo wa irabu /a/ na viyeyusho /y/ na /w/ katika Kiturkana. Mwinuko wa ulimi ni sifa bainifu za irabu kama inayojitokeza katika mizizi vifuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| - duk | jenga | - duk | jificha |
| - ger | vuna | - ger | chanja |

Irabu zilizo na sifa [ -mwinuko wa ulimi] huwa na sauti kali ilhali zile zilizo na sifa za [+ mwinuko wa ulimi] husikika kwa mpumuo. Irabu (-kaze) katika Kiturkana husikika kama kali. Irabu /ɛ/ na /ɔ/ husikika katika mifano fulani maalum na katika mazingira

fulani maalum. Ushahidi wa kisinkronia na wa kidiakronia unaonyesha kwamba vokali hizi zina asili mbili kama mfano ufuatao:

a) Vokali (-kaze) ambayo hubadilika na kuwa (+kaze) katika mazingira ya usilimisho. Mfano: -iryɔ → [iry] eusi

b) Irabu ya mbele juu ikiungana na /o/, ikifuatwa na mofimu iliyo na irabu ( -kaze). Kwa mfano:

Bun-i-o-r ε → [buner ε] njoo

Vokali /o/ na /e/ huwa kaze wakati ambapo zinatokea katika mofimu na kama silabi tangulizi ina irabu (-kaze) ya kati hivi kubadilika na irabu (+kaze) ya kati. Kwa mfano:

A – won- o-erɛ → [awonerɛ]

Kiturkana kina irabu refu ambazo hukizana na irabu fupi japo kuna chache huweza kutokea katika jozi kwa mfano:

Jik ‘ kabisa’

Jiik ‘kila mara’

Vile vile irabu refu katika Kiturkana inaweza kuwa na toni sambamba, inayopanda au inayoshuka. Kwa mfano:

A-t**aa** nyanya

mɛɛrɛ hapana

`ɛ-m`aa`ni` fahali

ɛ-k**aa**l ngamia

Pia ifahamike kwamba ni nadra katika Kiturkana kupata irabu refu isiyosikika yenye toni ya chini. Irabu hizi mara nyingi huonekana zimetokana na mfuatano wa mofimu mbili

katika neno husika. Irabu refu katika Kiturkana kabla ya kutua hufupishwa hususan wakati ambapo kipasuo /p/ kinatokea mwishoni mwa neno kwa mfano:

a-pɔɔ → [apɔ?]

Irabu hafifu au isoghuna katika Kiturkana mara nyingi huwa za juu japo kuna zile za chini. Vilevile kuhusu nafasi ya irabu hafifu au isoghuna katika neno aghalabu huwa mwishoni wa neno. Hata hivyo irabu au vokali ghuna pia hutokea mwishoni wa neno. Kwa mfano:

/akimij**a** / → [akimija] tengeneza.

Irabu za Kiturkana hudondoshwa kabla ya irabu ya aina moja wakati mpaka wa mofimu inaingilia kati. Udondoshaji huu hutokea tu vokali za katikati ya neno. Kanuni ya udondoshaji huu ni:

i →Ø / → - i

Mfano wa udondoshaji wa irabu ni:

[a-ki-iti-idɛt ] →[ak-it-idɛt]

Usilimishwe wa Irabu katika Kiturkana hutokea pale ambapo irabu inayotangulia au inayofuata nyingine inasilimishwa kabisa. Ni vyema ifahamike kwamba usilimisho kabisa wa irabu ni tofauti na uwiano wa irabu. Hii ni kwa sababu ni mchakato wa kiwango chini wa kifonetiki. Mara nyinyi viambishi awali husilimishwa na mzizi. Vokali huweza kuwa tofauti nyingine kulingana na sifa za kifonolojia. Kwa hivyo irabu yenye sifa [+ juu, -nyuma] huweza kubadilika na kuwa [+juu, -nyuma] kwa mfano:

k-imuj → [ kumuj] kula

Vile vile irabu yenye sifa ya [- juu, - chini] huweza kuwa [-juu, +chini] kwa mfano

tɔ- tac → [tatac] lipa

tɔ-mat → [tamat ] kunywa

Mifano ya maneno yaliyo na irabu za Kiturkana

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i)** | /**a**pa/ | [apa] | baba |
| | /ata:/ | [ ata:] | nyanya |
| | /akimij**a** / | [akimija] | |
| | tengeneza | | |
| **ii)** | **ɛ**paka | [ ɛpaka] | paka |
| | /am**ɛ**:i / | [amɛ:l] | meli |
| | /akital**ɛ**/ | [akital**ɛ**] | dumisha |
| | mila | | |
| iii) | /ɛlip**i** / | [ ɛlip**i** ] | omba |
| | /atikit/ | [ atikit] | tikiti |
| iv) | /alɔr/ | [alɔr/] | lori |
| | /akidɔŋ / | [ akidɔŋ] | baki |
| | / amutarɔ/ | [amutarɔ] | mtaro |
| v) | /ɛd**u**kan / | [ɛd**u**kan] | duka |
| | /akip**u**set | [ akip**u**set] | kifutio |

Irabu za Kiturkana zinaweza kupambanuliwa kwa kutumia vigezo vitatu:

a) Sehemu pa kutamkia katika ulimi

b) Mwinuko wa ulimi

c) Mkao wa mdomo.

Kwa muhtasari tunaweza kuonyesha sifa bainifu za irabu za Kiturkana kama ifuatavyo:

| /a/ | /ɛ/ | /ɛ:/ |
| --- | --- | --- |
| + irabu | + irabu | + irabu |
| +mbele | +mbele | + mbele |
| + chini | +mbele | + kati |
| -mviringo | + kati | - mviringo |
| -refu | -refu | - refu |

| /i/ | /i:/ | /ɔ/ | / ɔ:/ |
| --- | --- | --- | --- |
| + Irabu | +irabu | + irabu | + irabu |
| + mbele | +mbele | + nyuma | + nyuma |
| + juu | +juu | + nusujuu | + nusu-juu |
| - mviringo | - mviringo | + mviringo | + mviringo |
| -refu | + urefu | -refu | + refu |

| /u/ | /u:/ |
| --- | --- |
| + irabu | + irabu |
| + nyuma | + nyuma |
| +juu | + juu |
| +mviringo | + mviringo |
| -refu | + refu |

### 2.1.3 Fonimu za Konsonanti za Kiturkana

Kiturkana kina konsonanti kumi na sita. Konsonanti za Kiturkana zina sifa za [+konsonanti] na [-vokali]. Nazo viyeyusho vya Kiturkana sifa za [-Konsonanti] na [-vokali]. Tutaainisha konsonanti za Kiturkana kwa kuzingatia mahali pa kutamkia na namna zinavyotamkwa. Kwa kuzingatia mahali pa kutamkia, konsonanti tunapata konsonanti zifuatazo:

i) Mdomoni

Konsonanti zinazotamkwa mdomoni ni /p/, /b/, /m/ na /w/ ambayo ni kiyeyusho.

ii) Ufizi au masine

Konsonanti zinazotamkwa kwenye ufizi ni /d/, /t/, /s/, /z/ na /n/

iii) Kaakaa laini

Konsonanti za kaakaa laini ni /k/ , /g/ na /ŋ/

iv) Kaakaa gamu

Konsonanti zinazotamkwa kwenye kaakaa gumu ni /c/, /j/, /ɲ/ na /j/ ambayo ni kiyeyusho

Kiturkana kina aina zifuatazo za konsonanti kulingana na namna ya kuzitamka konsonanti husika:

**Vizuiwa**

Kiturkana kina vizuiwa sita. Vizuiwa hivi ni: /b/, /p/, /d/, / t/, /k/ na /g/. Wakati wa kutamka sauti hizi mkondo wa hewa hubanwa kabisa katika ala za kutamkia kisha kuachiliwa ghafla na kutoa sauti yenye mpasuo. Fonimu /p/ inaweza kukwamizwa inapotokea mwanzoni mwa silabi. Kwa mfano:

a-paa [ a.p$a] Kitanda

Fonimu /b/, /d/ ,/g/ zinaweza kubadili mahali pao kutamkiwa na kuwa za glota iwapo zitatokea mwanzoni mwa silabi.Kwa mfano: a-daar [a-da-a-r] nyara

Kwa upande mwingine zinapotokea mwishoni mwa silabi zinabaki kuwa vizuiwa ghuna. Kwa mfano: e-purot [ɛ-pu-rot] pombe

e- tid [ ɛ-tid] wengu

e-seg [ɛ-seg] safi

konsonanti /k/ hubadilika na kuwa konsonanti /g/ katika mazingira ya kufuatwa na vokali /a/ au /ɔ/. Mfano: mkate > [amugat]

mkokoteni > [amugɔgɔtɛ ni]

Mifano ya maneno ya Kiturkana yanayoundwa na vizuiwa ni :

| | | |
|---|---|---|
| /a**b**a/ | [aba] | baa |
| /a**p**a / | [aba] | baba |
| /daar/ | [daar/ | nyara |
| /gaar/ | [gaar] | gari |
| /paipai/ | [paipai] | papai |
| /taitai/ | [taitai ] | lowa |

Mifano tuliyobainisha ni jozi ya maneno yaliyouundwa kwa vizuiwa / b/ / p/ /d/ /k/ na /g/

**Vizuiwa kwamizwa**

Sauti za vizuiwa–kwamizwa ni sauti ambazo wakati wa kuzitamka hewa hufungiwa kabisa na ala za kutamkia kisha hewa kuachiliwa kupita kwa mlipuko japo ala za kutamkia haziachani kabisa ila huacha mwanya mdogo ambapo hewa huendelea kupita kwa kuwamizwa hivyo basi kusababisha mkwaruzo. Kina kina vizuiwa – kwamizwa viwili. Nazo ni : /c/ ambayo hutamkwa /tʃ/, na /ɟ/. Mifano ya maneno ya Kiturkana yaliyoundwa vizuiwa – kwamizwa ni kama vile :

| | | |
|---|---|---|
| /cɔrɔ/ | [cɔrɔ] | konde |
| /mcɛlɛ/ | [ɛmcɛlɛ] | mchele |
| /akimu**j**/ | [ akimu**j**] | chakula |

**Vikwamizwa**

Vikwamizwa ni sauti ambazo wakati wa kuzitamka ala za kutamkia hukaribiana kiasi kwamba mkondo wa hewa kusababisha mgusano unaosikika. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (1990), vikwamizwa ni sauti ambazo zikitamkwa, mkondo wa hewa hauzuiliwi kabisa ingawa ala za kutamkia zinakaribiana na kusababisha mkwaruzo fulani. Vikwamizwa vya Kiturkana ni /s/ na /z/. Kikwamizwa /s/ ni [-ghuna] lakini /z/ ni [+ghuna] na ni maneno machache sana katika Kiturkana yanayosheheni sauti /z/. Hii inatokana na hali hapo /z/ hubadilika na kuwa /s/ katika Kiturkana. Mifano ya maneno ya Kiturkana yaliyo na sauti /s/

Sapat mvulana

Salunit mwisho

Eseget bega

Neno lililo na sauti /z/ ni eszurroswara

Mifano nomino mkopo za Kiturkana zinazoundwa na vikwamizwa:

| | | | |
|---|---|---|---|
| / ɛsaa/ | > | [ɛsaa] | saa |
| /asɔkɔ/ | > | [asɔkɔn] | soko |
| /ŋimusaib/ | > | [ŋimusaib] | mzabibu |

**Nazali**

Nazali ni sauti ambazo hutamkwa wakati hewa huzuiliwa na kuachiliwa kupitia puani. Hewa inapozuiliwa mdomoni tunatamka /m/, ufizini /n/, kaakaa gumu /ɲ/ na kaakaa laini /ŋ/

Nazali /ɲ/ mara nyingi hudondoshwa wakati inatokea mwishoni mwa neno baada /o/ badala €

Kiturkana kina nazali nne. Nazali hizo ni **: /m/, /n/, /ŋ/, /ɲ/** . Nazali hizi huungana na irabu na hata na konsonanti nyingine kuunda nomino mkopo kama ifuatavyo:

/ɛ/+ /m/+/u/+ /c/+/ɛ/+ /l/+/ɛ/ > /ɛmucɛlɛ/

/a/+ **/ŋ/+/a/** +/s/ > /aŋas/

/ɛ/+/d/+/u/+/k/+/a/+/n/ > /ɛdukan/

/ɛ/+ /ɲ/+/ɛ/+/ɲ/+/a/ > /ɛɲɛɲa/

Mifano ya maneno ya Kiturkana yanayoundwa na nazali ni:

| | | |
|---|---|---|
| /mjɛkin/ | [mjɛkin] | wacha |
| /nakaapa/ | [nakaapa] | dada |
| /ŋidɛ/ | [ŋidɛ ] | watoto |
| /ɲas/ | [ ɲas ] | kima (nyama iliyosagwa) |

**Kitambaza**

Kiturkana kina kitambaza kimoja /l/. Kitambaza kinapotamkwa hewa huzuiliwa na kisha kuachiliwa kupita kando kando mwa ulimi wakati ambapo ulimi hugusana na ufizi . mifano ya maneno ya yenye fonimu hii ya kitambaza ni kama zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| /akilip/ | [akilip] | kuomba |
| /aliwaɛ/ | [aliwaɛ] | wapi |
| /ɲakimul/ | [ ɲakimul] | mate |

Nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili zinazoundwa na kitambaza ni kama ifuatavyo:

| **Kiturkana** | **Kiswahili** |
|---|---|
| /amɛɛl/ | meli |
| /ɛkalam / | kalamu |
| /ɛpilipili / | pilipili |

**Kimadende**

Kitambaza kinapotamkwa ncha ya ulimi hugusa ufizi huku hewa ikipita kati ya ncha ya ulimi inayopigapiga ufizi. Kiturkana kina kimadende kimoja tu. Kimadende hicho ni /r/ na huwa refu.

Mifano ya maneno yaliyo na kimadende:

| | | |
|---|---|---|
| /ɲabɛrr/ | [ ɲabɛrr] | wanawake |
| /ɛrɔt/ | [ ɛrɔt] | njia |

**Viyeyusho**

Viyeyusho vya Kiturkana ni /w/ na /j/ . Viyeyusho hivi vina sifa ya [-konsonanti] na [-vokali]. Hii ina maana kwamba vina sifa za konsonanti na za vokali. Viyeyusho huonyesha sifa za konsonanti zinapokuwa katika mfumo wa silabi ambapo huweza kuunda kiini cha silabi. Kwa kawaida vokali haiwezi kuunda kiini cha silabi mfano: a – ki- jɛp ⟶ [a.ki.jɛp]

Viyeyusho hudhihirisha sifa za vokali hususan katika uwiano wa vokali ambapo huonyesha sifa za mwinuko wa juu wa ulimi ambapo vokali inayotangulia kiyeyusho husika huwa ya mwinuko wa juu wa ulimi. Aidha viyeyusho huoneysha sifa za vokali wakati vinabeba toni hivyo basi kugeuka na kuwa vokali kamili /i/ na /u/

Viyeyusho vya Kiturkana hudondoshwa katika mazingira fulani maalum. Kwa mfano /w/ hudondoshwa ya mazingira silabi moja na vokali /u/

[w] → Ø / u

Mfano :

/ɛ-buw/ → [ɛ.buw] → [ɛbu] mnyama

Nayo /j/ hudondoshwa katika mazingira maalum ya kutanguliwa na vokali /i/ katika silabi moja.

[j] → Ø/ i

Kwa mfano:

-boy-i-kin [i-bo- ji-kin] → [ibokin] keti

Viyeyusho vya Kiturkana huundwa kutoka kwa vokali za juu katika mazingira fulani. Waaidha, kwa baadhi ya wazungumzaji wa Kiturkana, vokali /ɛ/ na /ɔ/ inakuwa viyeyusho kabla ya /a/ kama kanuni mbadala kwa mfano:

-ikɛ-ar → ikyaar kuinua

Kwa upande mwingine ikiwa silabi ya kifonetiki ni wazi, kizuiwa cha glota kinaweza kutokea. Kwa mfano: ɛ-pɛ-na → [epyana] Isio na ladha

Jedwali lifuatalo linatoa muhtasari ya aina za konsonanti za Kiturkana na mahali pa kutamkia.

Kielelezo cha jedwali: 3.1

| Aina za konsonanti | Midomo | Midomo na meno | Meno | Meno na ufizi | ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | glota | jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vizuiwa | /p/ /b/ | | | | /t/ /d/ | | /k/ /g/ | | 6 |
| Vizuio-kwamizo | | | | | | / c/ /ɟ/ | | | 2 |
| vikwamizo | | | | | /s/ /z/ | | | | 2 |
| Nazali | /m/ | | | | /n/ | /ɲ/ | /ŋ/ | | 4 |
| Kitambaza | | | | | /l/ | | | | 1 |
| Kimadende | | | | | /r/ | | | | 1 |
| Nusu–irabu | /w/ | | | | | /j/ | | | |

**Hitimisho kuhusu fonimu za Kiturkana**

Ni bayana kwamba Kiturkana kina konsonanti kumi na sita, viyeyusho viwili na irabu tisa japo zile nyingine tisa ni alafoni.Hata hivyo kuna sauti ambazo unazalishwa awali ambazo hatujaziorodhesha kama konsonanti za Kiturkana. Hii ni kwa sababu sauti hizi

mbili zinachukualiwa na baadhi ya wanaisimu kama Carl Meinhof kama mofimu ambatano badala ya kutamkwa kama fonimu moja. Fonimu hizi zinazonazalishwa awali katika Kiturkana ni mbili yaani: /mb/ na /nd/. Sauti hizi mbili zinapatika katika nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili kama ifuatavyo:

i) /akitambara/ kitambaa

ii) / ɛkitanda / kitanda

Ni dhahiri shahiri kwamba Kiturkana kina irabu tisa tofauti na Kiswahili kilicho na irabu tano tu.Vile vile Kiturkana hakina konsonanti ambazo ni zipo katika Kiswahili kama vile /f/, /v/ /sh/, /ch/ na /ng'/

## 2.2 Silabi za Kiturkana

Silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho kwa kawaida huwa kikubwa kuliko fonimu na kidogo kuliko neno. Silabi ni mwambatano wa fonimu ambazo huweza kutamkwa kama kitu kimoja. Silabi ya Kiturkana ina sehemu tatu yaani mwanzo, kilele na koda na kwamba kila silabi huwa na irabu kama kilele chake. Kiini ni sehemu ya silabi ambayo huwa katikati mwa silabi na husikika kwa nguvu zaidi kuliko sehemu ya mwanzo na sehemu ya mwisho ya silabi. Sehemu ya mwanzo na mwisho huweka mipaka kati ya silabi zinazofuatana katika neno. Sehemu ya mwanzo ya silabi huundwa kwa konsonanti au kiyeyusho Katika Kiturkana kama ilivyo katika lugha nyingi za ulimwengu, kuna hali ya wazungumzaji wa Kiturkana kuepuka silabi isiyo na sehemu ya mwanzo kwa kuchopeka kizuiwa cha glota wakati wa kutamka maneno ambayo sehemu ya mwanzo ya

silabi ya neno husika imenaza kwa Irabu. Sehemu ya mwisho ya silabi huweza kuundwa kwa kiyeyusho ama konsonanti au iliyotanguka.

Kwa vile kazi yetu inashughulikia mabadiliko ya kifonolojia, inatujuzu kushughulikia miundo ya silabi za Kiturkana. Isitoshe, nadharia tunayotumia katika utafiti huu yaani nadharia ya fonolojia zalishi asilia (NFZA), inaeleza kwamba usilabi ni kiambajengo muhimu katika kanuni ya mofolojia. kwa hivyo inatujuzu kushughulikia miundo ya silabi za Kiturkana.

### 2.2.1 Miundo ya silabi ya Kiturkana

Lugha mbalimbali huwa na miundo tofauti tofauti za silabi. Kazi yetu imebaini kwamba Kiturkana kina miundo ya silabi zifuatazo:

**i) Muundo wa silabi wa Konsonanti Irabu (KI)**

Muundo wa silabi wa konsonanti Irabu (KI) ndio muundo ambao wataalamu wengi wanauitwa muundo pendwa wa silabi. Kwa mfano, Iribemwangi (2008) anauita muundo wa silabi muundo unaopendelewa. Naye Hooper (1976), muundo ulio sahili zaidi katika masharti ya miundo ya silabi ni muundo wa KI. Wazo hili linauungwa mkono na Mgullu (1999) kwa kudai kwamba muundo wa konsonanti Irabu (KI) ndio unaopendelewa zaidi si tu katika lugha ya Kiswahili bali katika lugha zote za duniani. Katika lugha ya Kiturkana muundo unajtokeza katika maneno mengi ya Kiturkana. Kwa mfano:

| Neno | Muundo wa silabi | Maana |
|---|---|---|
| /lɔci/ | KI$K I | Mdogo |
| / ɲidɛ / | KI$KI | Watoto |
| /kuju/ | KI$KI | Kaskazini |
| /kide/ | KI$KI | Mashariki |

Muundo wa silabi wa Konsonanti Irabu unapatika maneno mengi katika Kiturkana ambapo mojawapo ya silabi katika neno huwa na muundo wa Konsonanti Irabu.

**ii) Muundo wa silabi wa Irabu (I)**

Kiturkana kina maneno mengi yaliyo na silabi ya Irabu pekee. Hapa ni pale ambapo kuna silabi ambayo ni irabu. Hii ni kwa sababu irabu /a/ na /e/ ndizo ambazo huchopekwa mwanzoni mwa maneno mengi hususan nomino aghalabu kudhihirisha jinsia ya kike na kiume mtawalia. Aidha kuna irabu /i/ ambayo pia huchopekwa mwanzoni mwa neno kuonyesha udogo wa nomino. Pia muundo pia wa irabu pekee waweza kutokea katikati mwa neno. Mifano ya maneno yenye silabi za irabu (I) ni kama ifuatavyo:

| Neno | Muundo wa silabi | Maana |
|---|---|---|
| /**a**kimuɟ/ | I$KI$KI$K | Chakula |
| /**ɛ**kilɛ/ | I$KI$KI | Mwanaume |
| /**a**mina/ | I$KI$KI | Upendo |

| | | |
|---|---|---|
| /Imεsik/ | I$KI$KI$K | Mwanakondoo |
| /**a**pa/ | I$KI | baba |
| /**εa**pεi/ | **I$I**$KI$I | pamoja |

Nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili huchopekwa irabu /ε/ au /a/ ili kubainisha nomino husika katika jinsia ya kiume au kike. Irabu /ε/ na /a/ hufanya kazi irabu kama silabi yenye muundo wa irabu.

iii) **Muundo wa silabi wa konsonanti konsonanti Irabu (KKI)**

Kiturkana kina muundo wa silabi ambao ni konsonanti, konsonanti Irabu. Kama iliyo kwa Kiswahili, si konsonanti zote za Kiturkana ambazo huungana na kuunda silabi hii. Konsonanti ambazo hushiriki katika kuunda muundo huu ni za nazali na kizuiwa kwamizwa /ɟ/. Maneno ya Kiturkana ambayo yana muundo huu wa silabi ni nomino mkopo za Kiswahili. Mifano ya maneno yaliyo na muundo wa KKI

| **Neno** | **Muundo wa silabi** | **Maana** |
|---|---|---|
| /εkita**nda**/ | I$KI$KI$**KKI** | Kitanda |
| /akitεndε/ | I$KI$KI$**KKI** | Kitende |
| /atambi/ | I$KI$**KKI** | Utambi |
| /acumpi/ | I$KI$**KKI** | Chumpi |
| /akambi/ | I$KI$**KKI** | Kambi |

Muundo wa silabi wa KKI hupatika katika nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili ambazo nazali hutangulia kizuiwa katika mazingira ya silabi moja. Hata hivyo nomino mkopo za Kiturkana ambayo nazali hutangulia kizuiwa katika mazingira ya silabi tofauti katika neno moja hazina muundo huu wa silabi. Kwa mfano:

| Neno | Muundo wa silabi | Maana |
|---|---|---|
| /ɛdis/ | I$KI$K | ndizi |
| /amugatɛ/ | I$KI$KI$KI | mkate |
| /ɛbɔka / | I$KI$KI | mboga |

**iv) Muundo wa silabi wa konsonanti pekee (K)**

Muundo wa silabi unaundwa kwa konsonanti. Katika Kiturkana kuna maneno mengi ambayo yaliyo na silabi ya konsonanti. Silabi hii mara nyinyi huwa mwishoni mwa neno tofauti na ya Kiswahili inatokea mwanzoni wa neno. IribeMwangi (2008) anasema kwamba muundo wa K katika Kiswahili ni wa nazali za mdomoni au za ufizi. Katika Kiturkana silabi hii ya K inaweza kuwa fonimu zozote zile.

Mifano ya maneno ya Kiturkana yenye muundo wa silabi za ( K)

| Neno | Muundo wa silabi | Maana |
|---|---|---|
| /kɔlɔ**ŋ**/ | KI$KI$**K** | Zamani |
| /tɔli**m**/ | KI$KI$**K** | Sema |
| /akita**b**/ | I$KI$KI$**K** | Kitabu |

v) **Muundo wa silabi wa konsonanti irabu irabu (KII)**

| Neno | Muundo wa Silabi | Maana |
|---|---|---|
| /tɔːma / | KI$I$KI | Ndani |

**vi) Muundo wa silabi funge**

Kiturkana kina silabi ambayo ni funge yaani silabi hii huishia kwa konsonanti. Mifano ya maneno ya Kiturkana yaliyo na silabi funge.

| Neno | Muundo wa silabi | Maana |
|---|---|---|
| /ɛkapɔl**ɔn/** | I$KI$KI$**KIK** | Mkuu |
| /ɛkata**man**/ | I$KI$KI$**KIK** | Mwalimu |

**vii) Muundo wa silabi wa konsonanti Nusu-Irabu Irabu ( K ½II)**

Katika uchunguzi wetu tumebaini kwamba kuna maneno katika Kiturkana ambayo yana muundo wa silabi wa konsonanti nusu-irabu irabu ( K ½II). Silabi hizi huundwa kwa konsonanti, nusu irabu na irabu. Mifano :

| Neno | Muundo wa silabi | Maana |
|---|---|---|
| /idja/ | I$K½II | Mwana |
| /akwar/ | I$K ½II$K | Siku |

**viii) Muundo wa silabi wa I ½II**

Tumetambua kwamba Kiturkana kina maneno yaliyo na silabi ya Irabu, nusu irabu kisha irabu.

| Neno | Muundo wa silabi | Maana |
|---|---|---|
| /awi/ | I$ ½II | Nyumbani |
| /ɛjauni/ | I$ ½II$I$KI | Ataleta |

Katika sehemu hii tumeshughulikia silabi ya Kiturkana na tumebaini kwamba kuna miundo minane ya silabi tofauti na Kiswahili iliyo na miundo tisa ya silabi. Muundo wa KKKI wa Kiswahili ndio haupo katika Kiswahili. Miundo ya silabi itatufaa sana kuelewa mabadiliko ya kifonolojia ambayo konsonanti na irabu ya nomino za Kiswahili hupitia zinapoingizwa katika Kiturkana.

**Hitimisho**

Katika sura hii tumeainisha fonimu za Kiturkana na tumebaini kwamba Kiturkana kina irabu tisa za kimsingi na zile nyingine tisa ni alofoni. Pia tumebaini kwamba Kiturkana kina konsonanti kumi na sita na nusu-irabu mbili. Aidha katika sura hii tumeshughulikia miundo ya silabi ya Kiturkana ambapo tumebaini kwamba Kiturkana kina miundo minane ya silabi. Katika kushughulikia fonimu za Kiturkana, miundo ya silabi na ngeli ya nomino za Kiturkana, tumefaulu kufahamu sarufi ya Kiturkana hivi kwamba itakuwa rahisi kufahamu mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

# SURA YA TATU

## 3.0 MABADILIKO YA KIFONOLOJIA YA KONSONANTI ZA NOMINO MKOPO ZA KITURKANA KUTOKA KISWAHILI

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tutajadili mabadiliko ya kimofofonolojia ambayo konsonanti za nomino za Kiswahili hupitia wakati zinakopwa na Kiturkana. Kwa kuwa tulishughulikia fonimu za konsonanti za Kiturkana katika sura ya pili ambapo tulibaini namna ambavyo zinatamkwa na mahali pa kutamkia. Kwa hivyo itakuwa rahisi kwetu kubaini mabadiliko ambayo konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hupitia ndipo zikubalike katika mfumo wa fonolojia ya Kiturkana.

Katika kutazama mabadiliko hayo tutaongozwa na vigezo vifuatavyo:

i) Konsonanti inayobadilika.

ii) Mabadiliko ya konsonanti yanayotokea.

iii) Motisha ya mabadiliko hayo ya konsonanti.

iv) Upeo mabadiliko ya konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana.

Aidha, nadharia tunayotumia katika utafiti wetu yaani nadharia ya fonolojia zalishi asilia (NFZA) itatusaidia kubaini sheria zinazoelekeza mabadiliko ya kifonolojia ambayo konsonanti za Kiswahili hupitia ndipo zikubalike katika Kiturkana. Hii ni kwa sababu nadharia ya fonolojia zalishi asilia ina kanuni nne ambazo ni kanuni za kifonetiki yaani kanuni ya 'P'. Kanuni hii ya P hufanya kazi katika maneno mkopo kutoka lugha nyingine. Aidha, kanuni hii ya P huweka mipaka kati ya silabi na mwisho wa neno. Hii ina maana kwamba kanuni hii ya P inatufaa sana katika kufafanua mabadiliko ya sauti

kama udhoofikaji, usilimisho, uchopekaji wa sauti. Kanuni nyingine ni Kanuni ya mofolojia itatusaidia kufahamu kuelewa mabadiliko ya kifonolojia katika mazingira kimofolojia. Aidha kanuni ya Via itatuwezesha kutambua mabadiliko ya sauti za Konsonanti za Kiturkana . Hatimaye kanuni ya Sandhi itatuelekeza kuelezea mabadiliko yalipo kati ya silabi na neno. Hii ni kwa sababu baadhi ya konsonanti zitabadilika ili kuafiki silabi ya lugha pokezi.

Katika sura hii vilevile tutadhihirisha muundo ndani na muundo wa nje kama anavyosema Hooper (1976) kwamba miundo ndani hudhihirika katika miundo nje ya maneno. Katika kuelezea miundo ndani na miundo nje tutazingatia mawazo ya Hyman (1975) kwamba katika mabadiliko ya kifonolojia, ni lazima kuzingatia uwezekano wa kubashirika, iktisadi ya vipashio, uwiano wa ruwaza na uasilia. Kulingana na Hyman (1975), lazima kuwe na uwezekano wa kubashiri ni muundo ndani upi unaweza kujitokeza kutokana na muundo nje wa neno hususan katika mazingira ya kipashio husika. Kwa mfano katika Kiturkana kiyeyusho /w/ hudondoshwa katika nomino ebuw na kuwa ebu.

/ɛ-buw/ → [ɛ.buw] → [ɛbu]

Iktisadi ya vipashio ni mchakato ambao unaohusu matumizi ya vipashio vichache kwa mfano nomino ya Kiturkana */ɛkilɛ/* ina vipashio vichache kuliko wingi wake */ŋikiljɔk/*
Uwiano wa ruwaza ina maana kwamba kuna sauti ambazo zinapatika katika lugha fulani na zile ambazo hazipatikani katika lugha hiyo husika. Kwa mfano katika Kiturkana

hakuna sauti /f/ /v/ /x/ /h/ na kadhalika. Kwa hivyo sauti hizi hudondoshwa ili kusahilisha utamkaji katika Kiturkana.

Mifanyiko ya kimofofonolojia kama vile usilimisho na uwaiano katika Kiturkana hujiri wakati nomino za Kiswahili zinakopwa na Kiturkana ili kupata muundo mwafka wa silabi. hivi basi kuafiki mawazo ya Schane ( 1975) aliyezigawa kanuni ya uasilia katika vitengo vitatu vikuu yaani kanuni ya uwiano au usilimisho, kanuni ya muundo mwafaka wa silabi na kanuni ya kutengana kwa sauti iwezekanavyo.

## 3.2 Mifanyiko ya kimofofonolojia ya konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana

Nomino za Kiswahili zinapokopwa na Kiturkana, konsonanti zake hupitia mabadiliko mbalimbali ya kimofofonolojia ndipo zikubalike katika Kiturkana. Mifanyiko hii ni kama ifuatavyo:

### 3.2.1 Kudhoofika kwa konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana

Mgullu (2010) anaeleza udhoofikaji wa fonimu kama ile hali ya fonimu fulani kubadilika kutoka fonimu ambayo hutamkwa kwa nguvu zaidi na kuwa sauti ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo kuliko ile ya awali. Kwa hivyo kudhoofika kwa sauti hujiri pale ambapo nguvu chache za msuli wa ala za sauti na msukumo mdogo wa mkondohewa hutumika kutamka alofoni kuliko kutamka fonimu. Katika Kiswahili kudhoofika kwa konsonanti mara nyingi huhusisha kugeuka kwa konsonanti za vipasuo na kuwa za vikwamizwa. Naye Iribemwangi (2008) akimdara na Polome (1967) anayedai

kwamba fonimu za vizuiwa vya Kiswahili hudhoofika wakati vinatokea kabla ya vokali /i/ wakati wa unomishaji wa vitenzi vyenye asili za kibantu.

Udhoofikaji wa konsonanti hutokea katika lugha ya Kiturkana. Kwa mfano Leiden (1983) anadai kwamba konsonanti /k/ ambayo ni kizuiwa [-ghuna) inadhoofika na kuwa kizuiwa /g/ [+ghuna] cha kaakaa laini wakati inapozingiriwa na vokali /o/ ua /a/ iliyo katika silabi moja na konsonanti /k/. Leiden anatoa mfano huu:

Na-bɔkɔbɔk → [na.bɔ.kɔkɔg] ngozi ya ndovu

Konsonanti /k/ ya baadhi ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hudhoofika wakati ambapo nomino mkopo hizo zinaingizwa katika Kiturkana. Kwa mfano konsonanti /k/ hubadilika na kuwa /ŋ/ katika mazingira ambapo Konsonanti /k/ hufuatwa na vokali [i] ilmuradi vokali hiyo imo katika silabi moja na konsonanti /k/. Kwa mfano:

| **Nomino ya Kiswahili** | | **Kiturkana** |
|---|---|---|
| Kiswahili | > | [ŋaswahili] |
| Kiarabu | > | [ ŋaarabu ] |
| Kizungu | > | [ŋamusungui] |

Kutokana na mifano hii, sheria ifuatayo inaweza kuundwa :

[+mpasuo] > [- mpasuo] – /vokali [i]

Sheria ni :

/k/ > [ŋ] — / vokali [i]

Sheria hii inaweza kufafanuliwa kwamba konsonanti /k/ inabadilika na kuwa /ŋ/ katika mazingira ya kufuatwa na vokali /i/. Vilevile konsonanti /k/ hubadilika na kuwa /g/ katika mazingira ya kufuatwa na vokali /a/ au /ɔ/

| **Nomino ya Kiswahili** | | **Kiturkana** |
|---|---|---|
| /mkatɛ/ | > | [ amugati] |
| /mkahawa/ | > | [ɛ mugaan] |
| /mk ɔ k ɔ t ɛ ni/ | > | [emug ɔ k ɔ t ɛ n] |

Kutokana na mifano hii, sheria inaweza kuundwa kama ifuatavyo:

/k/ > [ g] / - vokali [a au ɔ]

Sheria hii inaweza kufafanuliwa kwamba konsonanti /k/ inadhoofika kuwa konsonanti /g/ katika mazingira ya kufuatwa na vokali /a/ au /ɔ/.

Konsonanti /z/ [+ghuna] hudhoofika na kuwa /s/ [-ghuna] wakati nomino za Kiswahili zinakopwa na Kiturkana. Mifano:

| **Kiswahili** | | **Kiturkana** |
|---|---|---|
| /kiazi/ | > | [ɛbias] |
| /mzungu / | > | [ɛmusuŋut] |

Nomino mkopo nyingi zilizo na konsonanti /z/ zinapokopwa na Kiturkana zinabadilika na kuwa /s/. Hii ni kwa sababu maneno machache sana ya Kiturkana yaliyo na konsonanti /z/ kama tuliyoeleza katika sura ya pili.

### 3.2.2 Kuimarika kwa konsonanti

Kuimarika kwa konsonanti hutokea pale ambapo alofoni za sauti fulani hutamkwa kwa nguvu nyingi na ala sauti kuliko wakati wa kutoa sauti yenyewe. Konsonanti za nomino

za Kiswahili huimarika wakati zinaingizwa katika Kiturkana. Kuimarika huku kwa konsonanti za nomino za Kiswahili zinapokopwa na Kiturkana hubadilisha namna ya kutamka na mahali pa kutamkia konsonanti inayoimarika. Konsonanti /f/ ambayo ni kikwamizwa cha meno na ufizi, huimarika na kuwa kipasuo / p/ kinachotamkwa mdomoni. Sauti /f/ ambayo ni kikwamizwa hafifu yaani isiyo ghuna inaimarika na kuwa kipasuo /p/ hafifu isiyo ghuna na inayotumia nguvu nyingi kutamka. Mifano ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili ambazo konsonanti /f/ inaimarika ni kama ifuatavyo:

ɛlfu > /ɛ+lf+u/ > [aluput]

askofu > /a+skɔ+fu/ > [askop]

Katika nomino hizi mbili tunaona kwamba iwapo silabi ya mwisho ya nomino ina silabi **fu** basi /f/ humairika kuwa /p/ huku irabu /u/ ikidondoshwa. Hata hivyo iwapo silabi ya mwisho si **fu** basi irabu ya mwisho ya silabi hiyo husika haidondoshwi

/Kufuli/ > [akipuli]

/bɔfulɔ/ > [abɔfulɔ]

/kɔfia/ > [akɔpia]

Tunaweza kuunda kanuni kuelezea mabadiliko haya kama ifuatavyo:

/ f/ > [p] / —/u/

Vilevile sauti / f/ ya kikwamizwa huimarika na kuwa kipasuo [p] katika mazingira ya kutangulia vokali /i/ kwa mfano:

kwa hivyo sheria ni /f/ > [p] —/i/

Mabadiliko haya mawili ya kuimarika kwa vikwamizwa na kuwa vipasuo katika nomino mkopo za Kiturkana yaweza kujumuishwa kwa sheria ifuatayo:

/f/ > [p] – /u na i/

Hii ina maana kwamba konsonanti /f/ ambayo ni kikwamizwa kinabadilika na kuwa /p/ ambayo ni kipasuo kinachotumia nguvu nyingi kutamka. Sheria hii inadhihirishwa kama ifuatavyo:

| Nomino ya ksiwahili | Ishara ya IPA | Nomino mkopo ya Kiturkana | Ishara ya IPA |
|---|---|---|---|
| Elfu | [ɛlfu] | elupu | [ɛlupu] |
| Kufuli | [kufuli] | ekupul | [ɛkupul] |
| Boflu | [bɔflu] | abopulo | [abupulɔ] |
| Kofia | [kɔfia] | akopia | [akɔpia] |

### 3 .2.3 Kudondoshwa kwa konsonanti

Baadhi konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hudondoshwa zinapoingia katika Kiturkana. Kutokana na data tuliyokusanya kutoka kwa Bibilia ya Kiturkana, Misali ya Kiturkana na Kamusi ya Kiingereza — Kiturkana, konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana zinazodhihirisha udondoshaji ni kama zifuatazo:

### 3.2.4 Udondoshaji wa /m/

Nazali /m/ inapofuatwa na kizuiwa katika mazingira ya silabi moja ambapo silabi hiyo huwa ya kwanza ya nomino ya Kiswahili hudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu ya /ɛ/. Mabadiliko haya ya kimofofonolojia tunaweza kuyasawiri kama yafuatayo:

i) [mbɔga] > / e+bɔka/ > [ɛbɔka]

Kutokana na mchakato huu tunaweza kubuni kanuni ifuatayo:

/mbɔga / > / [ ɛbɔka]

/m/ > b/ — [ɛ]

$$\underset{/m/}{\begin{bmatrix} +\text{kons} \\ +\text{nazali} \\ +\text{mdomo} \\ +\text{ghuna} \end{bmatrix}} > \underset{/b/}{\begin{bmatrix} +\text{kons} \\ +\text{mdomo} \\ -\text{nazali} \\ +\text{ghuna} \end{bmatrix}} + \underset{/\varepsilon/}{\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{irabu} \end{bmatrix}}$$

Katika kanuni hii, nazali /m/ ambayo hutamkiwa mdomoni hudondoshwa wakati inafutwa na kipasuo / b/ cha mdomoni ambayo ni ghuna na nafasi yakekuchopekwa vokali / ɛ/. Motisha ya mabadiliko haya ni kurahisisha utamkaji kwa sababu tunapata muundo wa silabi ya irabu pekee.

Pia nazali /m/ hudondoshwa katika mazingira ya kufuatwa na kipasuo au kizuiwa /p/ ambacho hutamkwa mdomoni ,isiyo ghuna na haina sifa bainifu ya unazali. Irabu /ɛ/

huchukua nafasi ya nazali ili kupata silabi ya irabu pekee itakayosahilisha utamkaji wa nomino hii mkopo ya Kiturkana.

ii) /mpira/ > [epira]

/m/ > p/ -[ɛ]

| /m/ | | /p/ | | / ɛ/ |
|---|---|---|---|---|
| +kons | | + kons | | |
| +nazali | > | + kizuiwa | + | + silabi |
| + mdomo | | -nazali | | +irabu |
| +ghuna | | - ghuna | | |

Ni bayana kwamba udondoshaji wa /m/ haifuati sheria ya Ganda kwani katika Kiturkana nazali /m/ ndiyo inayodondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu /ɛ/

### 3.2.5 Udondoshaji wa /n/

Konsonanti /n/ hudondoshwa katika mazingira ya kufuatwa na konsonanti /d/ katika silabi ya mwanzoni mwa neno. Baada ya nazali /n/ kudondoshwa nafasi yake huchopekwa irabu / ɛ/ au /a/ ili kuleta muundo wa silabi ya irabu pekee. Aidha, vokali / ɛ/ au /a/ inayochopekwa baada ya kudondoshwa kwa nazali /n/ huwakilisha mofu ya jinsia ya kiume na kike mtawalia. Ifahamike kwamba nomino za Kiturkana huchukua jinsia ya kiume au kike.

Mifano

i) /ndizi/ > [ɛdis]

ii) /ndɔ:/ > [ɛdɔ:]

iii) /ndimu/ > [adimu]

Mabadiliko haya tunaweza kuyadhihirisha kwa sheria ifuatayo:

/n/ > [$^{\theta}$ ] / -d

Sheria hii inaonyesha kwamba konsonanti /n/ ya nomino ya Kiswahili inadondoshwa katika mazingira ya kufuatwa na konsonanti /d/ wakati konsonanti /n/ na /d/ zipo katika silabi moja ya mwanzoni mwa nomino ya Kiswahili. Hata hivyo sauti /n/ haiwezi kudondoshwa inapofuatwa na konsonanti /d/ katika silabi moja mwishoni mwa nomino. Kwa mfano katika maneno kama /kitanda/ na /kitende/

/kitanda/ > [ɛkitanda]

/kitɛndɛ/ > [ ɛkitɛndɛ]

Udondoshwa wa nazali /n/ ya ufizi katika mchakato huu ni kupata silabi ya irabu pekee ili kusahilisha utamkaji wa nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Aidha, irabu /ɛ/ au /a/ hudhihirisha mofimu ya jinsia ambayo nomino za Kiturkana huanishwa kijinsia. Kwa hivyo mchakato unamotishwa na kanuni ya kifonetiki na kanuni ya Via.

### 3.2.6 Udondoshaji wa /h/

Nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili zilizo na konsonanti /h/ hudhihirisha hudondoshaji wa konsonanti /h/ ambayo ni sauti ya kikwamizwa cha glota kisicho nazali na kisicho ghuna. Udondoshaji wa konsonanti /h/ hutokea kwa sababu haipo katika Kiturkana. Tukimdara Hyman (1975) anayedai kwamba katika mabadiliko ya

kifonolojia, ni lazima kuzingatia uwezekano wa kubashirika, iktisadi ya vipashio, uwiano wa ruwaza na uasilia. Hii ni kwa sababu ruwaza za sauti za lugha husika hujulikana na mzungumzaji wa lugha hiyo husika. Udondoshaji unadhihirishwa na mifano ifuatayo:

/Mtihani/ > [ɛmtiani]

/Sahani/ > [asani]

/hotɛli/ > [ɛotɛl]

Tunaweza kubuni kanuni ifuatayo kuelezea mchakato huu wa udondoshaji wa /h/

/h/ > [ Ø] /- k

Kanuni hii inaweza kufafanuliwa kwamba, konsonanti /h/ inadondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na irabu au kufuatwa na irabu.

Kwa vile Kiturkana hakina konsonanti /h/ inalazimu nomino mkopo iliyo na konsonanti/h/ kudondoshwa inapoingizwa katika Kiturkana ili kuafiki mfumo wa fonolojia ya Kiturkana.

### 3.2.7 Udondoshaji wa /j/

Kiyeyusho /j/ hudondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na irabu /a/ wakati nomino za Kiswahili zinapokopwa na Kiturkana. Udondoshaji wa kiyeyusho /j/ hutokea ili kuepuka silabi zisizo na mwanzo wa silabi.

Mfano :

/malaja/ > /amalaat/

Mchakato unaweza kuelezwa na kanuni ifuatayo:

/j/ > Ø / [a ]

Kanuni inaweza kuelezwa kwamba kiyeyusho /j/ hudondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na irabu /a/.

### 3.2.8 Udondoshaji /w/

Kiyeyusho /w/ inapotanguliwa na nazali katika mazingira ya silabi inayoanza na nazali kisha kufuatwa na /w/ katika silabi husika, /w/ hudondoshwa. Mifano:

| Kiswahili | | Kiturkana |
|---|---|---|
| /mwalimu/ | > | /ɛmaalimɔt/ |
| /mwaka/ | > | /ɛmaka/ |
| /machungwa/ | > | /amacugat/ |

Tunaweza kubuni kanuni hii:

/w/ > Ø / [m au ɳ]

Mfanyiko huu una maana kwamba nusu-irabu /w/ inadondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na nazali /m/ au /ɳ/ katika mawanda ya silabi moja. Mfanyiko huu hujiri ili kuepuka silabi isiyo na mwanzo.

## 3.3 Uchopekaji wa konsonanti

Mabadiliko mengine ambayo nomino za Kiswahili hupitia wakati zinapokopwa na Kiturkana ni uchopekaji wa konsonanti. Baadhi ya uchopekaji wa konsonanti katika nomino za Kiswahili zinazokopwa na Kiturkana zinamotishwa kifonolojia na nyingine kumotishwa kimofolojia. Uchopekaji ambao unamotishwa kifonolojia ni pale ambapo konsonanti inachopekwa kwenye nomino mkopo ili iafike mfumo wa fonolojia ya Kiturkana. Uchopekaji konsonanti ambao unamotishwa kimofolojia ni ule ambao unaletwa na kuchopekwa kwa konsonanti kwenye nomino mkopo ili ikubalike kwenye mofolojia ya Kiturkana. Katika mchakato wa uchopekaji wa konsonanti kwenye nomino za Kiswahili zinapokopwa na Kiturkana ni kama ifuatayo:

Uchopekaji wa konsonanti /t/ hutokea mwishoni wa nomino mkopo za Kiturkana kama kwenye nomino za Kiswahili zifuatazo:

| **Kiswahili** | | **Kiturkana** |
|---|---|---|
| /mzungu/ | > | [ɛmuzungut] |
| /mia / | > | [ amiat] |
| /malaya/ | > | [amala:t] |
| /magadi / | > | [ amakat ] |
| /malaika / | > | [ ɛmalaikat] |
| /elfu / | > | [ aluput ] |

Mabadiliko yanayotokea wakati konsonanti inachopekwa kwenye nomino mkopo za Kiswahili ni yale ambayo yanamotishwa kifonolojia na kimofolojia. Hii ina maana kwamba kipasuo cha mdomo /t/ kinachopekwa mwishoni mwa nomino mkopo za Kiturkana ili kusahilisha utamkaji na kwa wakati uo huo kupata muundo wa silabi ya silabi funge kama tulitazama katika sura ya pili.

### 3.3.1 Uchopekaji wa /n/

Katika data yetu kuna baadhi ya nomino za Kiswahili zinapokopwa na Kiturkana huchopekwa konsonanti /n/ ambayo ni nazali ya ufizi iliyo ghuna mwishoni mwa nomino mkopo ya Kiturkana kutoka Kiswahili ili kusahilisha utamkaji wake. Uchopekaji huu unamotishwa kifonolojia kwani uchopekaji wa nazali /n/ kuunda mfumo wa fonolojia inayokubalikana katika Kiturkana. Aidha uchopekaji unamotishwa kimofolojia kwani inaleta muundo wa silabi wa silabi funge yaani Konsonanti Irabu Konsonanti.

Nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili zinazosawiri mageuzi ya uchopekaji wa konsonanti ni :

| **Kiswahili** | | **Kiturkana** | **Othografia** |
|---|---|---|---|
| Soko | > | [asɔkɔn] | asokon |
| Duka | > | [ɛdukan] | edukan |

### 3.4 Usilimisho pamwe wa nazali

Usilimisho pamwe wa nazali ni mabadiliko ambayo hujiri wakati ambapo nazali hufuatwa na konsonanti isiyo nazali. Konsonanti ya nazali hubadilisha mahali pake pa kutamkwa na kutamkwa kwenye sehemu inayotamkiwa konsonanti husika inayoifuata. Schane (1973) anaeleza usilimisho pamwe wa nazali kama kanuni ya uwiano kwani kuna ukubaliano wa nazali na konsonanti isiyo ya nazali inayoifuata.Kuna baadhi za nomino za Kiswahili zinazodhihirisha usilimisho pamwe wa nazali wakati zinakopwa na Kiturkana. Kutokana na data tulichota kwenye kamusi ya Kiingereza – Kiturkana, Bibilia ya Kiturkana na misali ya Kiturkana nomino mkopo za Kiturkana zifuatazo zinadhihirisha usilimisho pamwe wa nazali:

| **Nomino ya Kiswahili** | | **Nomino mkopo ya Kiturkana** |
|---|---|---|
| Sanduku | > | [ asanduku] |
| Kitanda | > | [ ɛkitanda ] |
| Peremende | > | [ ɛpɛrɛmɛndɛ] |
| Chandarua | > | [ ɛtandarua ] |
| Gondoro | > | [ ɛkɔndɔrɔ] |

Katika nomino mkopo hizi za Kiturkana sauti /n/ na /d/ zinasilimishwa wakati zinaungana ili kurahisisha matamshi. Ni wazi kwamba sauti hizi mbili zinatamkiwa kwenye sehemu moja yaani kwenye ufizi. Kanuni ya mchakato huu ni kama ifuatavyo:

/n/ > / - /d/ [+ ufizi]

/N/ hutokea kama /n/ katika mazingira ya kufuatwa na /d/

Nomino mkopo [aŋas] ambapo nazali /n/ ya mbele huvutwa mbele na kikwamizwa /g/ ya kaakaa laini na kutamkwa kama /ŋ/ . Sheria ya badiliko linasawiriwa ifuatavyo:

/n/ > /ŋ/ — [+mbele]

[a + n+ gas] > [aɳas]

Vilevile nomino mkopo za Kiturkana [atambi] na [akambi] kutoka kwa nomino za Kiswahili 'utambi' na kambi mtawalia zinapitia mchakato huu wa usilimisho pamwe wa nazali. Katika mchakato huu nazali /m/ ambayo ni nazali ya mdomoni inabadilika na kukubaliana na /b/ ambayo ni kipasuo cha mdomo. Wakati wazungumzaji wa Kiturkana wanatamka maneno haya sauti /n/ huvutwa na /b/ na kutokea kama /mb/ ambayo hutamkiwa mdomoni. Tunaweza kusawiri mchakato huu wa usilimisho pamwe kwenye nomino mkopo za Kiturkana [atambi] na [akambi] kwa kanuni ifuatayo:

/n/ > m / - [+mdomo]

Utambi > /a+ta+n+bi/ > [atambi]

Kambi > /a + ka+ n+ bi/ > [akambi]

Mabadiliko haya ya usilimisho pamwe wa nazali yanayokumba nomino mkopo za Kiturkana ni ya kutabirika kwani sauti moja huathiriwa na nyingine. Aidha, mchakato huu unamotishwa kifonetiki kwani hukumba sauti fulani.

### 3.5 Ubadala wa konsonanti

Antilla (1972) anaeleza kwamba wazungumzaji wazawa wa lugha husika hufahamu sifa bainifu za fonolojia ya lugha yao. Na kwamba wakati maneno ya kigeni yaingizwa katika lugha yao wao huipa maneno hayo sauti zilizo karibu na ya lugha yao. Mawazo haya ya Antilla kwa kiwango fulani yanaungwa na mkono namna wazungumzaji wa Kiturkana wanavyobadilisha sauti ya nomino za Kiswahili ili nomino hizo mkopo zitamkwe kama Kiturkana. Kwa mfano:

i) firimbi > /ɛkapiriɳirit/ ekapiringit

Tunaweza kuunda kanuni hii kueleza mchakato huu kama ifuatavyo:

/mb/ > [ɳ ] / + / t/

Kanuni inamaanisha kwamba sauti inayonazalishwa awali /mb/ imepitia mifanyiko ya ubadala na kuwa nazali ya Kiturkana /ɳ/ katika mazingira ya kuchopekwa konsonanti /t/ ili kupata silabi funge ya Kiturkana.

ii) Kikombe > /ɛkɔpɔ/ > ekopo

Kanuni : /mb/ > [p] / + /i/

Kanuni ina maana kwamba sauti /p/ ya Kiturkana imetokana na ubadala na sauti inayonazalishwa awali ya Kiswahili katika mazingira ya kuchopekwa kwa irabu ya nyuma, nusu-chini na mviringi ili kupata muundo mwafaka wa silabi ya Kiturkana ya konsonanti irabu.

**Hitimisho**

Katika sura hii tumeshughulikia mabadiliko ya kifonolojia ambayo nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hupitia wakati zinapokopwa na Kiturkana. Mabadiliko hayo ni kama vile udhoofikaji wa konsonanti, umairikaji wa konsonanti, udondoshaji wa konsonanti, uchopekaji wa konsonanti, usilimishwe pamwe wa nazali na ubadala wa konsonanti. Mabadiliko haya ya konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana hutokea ili kuafiki fonimu ziliko katika Kiturkana na kupata muundo fulani wa silabi ili kusahilisha utamkaji nomino mkopo hizo.

## SURA YA NNE

## 4.0 MABADILIKO YA KIFONOLOJIA YA VOKALI ZA NOMINO MKOPO ZA KITURKANA

Katika sura hii tutashughulikia mabadiliko ya kifonolojia ambayo vokali za nomino za Kiswahili hupitia zinapokopwa na Kiturkana. Katika uchunguzi wa mifanyiko ya kifonolojia ya vokali za nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili, tutatumia vigezo kama tulivyotumia katika sura ya tatu kuchunguza mabadiliko ya konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili. Vigezo hivyo ni pamoja na:

i) Vokali inayobadilika.

ii) Vokali inayobadilika na kuwa nini au matokeo ya mabadiliko ya vokali husika.

iii) Motisha ya mabadiliko.

iv) Upeo wa mabadiliko hayo katika Kiturkana.

Katika kuchunguza mabadiliko haya kimofofonolojia ya irabu za nomino mkopo za Kiturkana tutajikita katika nadharia ya fonolojia zalishi asilia (NFZA) ambayo hudara fonolojia kwa upande mmoja na mofolojia kwa upande mwingine. Nadharia ya NFZA ina kanuni ya uasilia na kanuni ya ujumlishaji sahihi kama vile tulivyoona katika sura ya tatu wakati tulipokuwa tukishughulikia mabadiliko ya kifonolojia ya kononsanti za nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili. Kanuni hizi ni nne nazo ni:

Kanuni za ‘P’ zinazomotishwa kifonetiki huwa zalishi na sifa za ubia na hupatika katika lugha nyingi za ulimwengu na kwamba kanuni hufanya kazi katika maneno mkopo na katika uchunguzi wetu itahusu nomino mkopo za Kiturkana. Kanuni itasaidia katika

kueleza mabadiliko ya kifonolojia ambayo hukumba irabu ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Kanuni nyingine ni kanuni ya 'MP' au kanuni za mofolojia. kanuni hizi huhusisha kanuni za kifonolojia katika mazingira ya kimofolojia ambapo tutajikita katika nomino mkopo za Kiturkana. Kanuni nyingine ni za nadharia hii ni kanuni ya Via kanuni hizi zitatumiwa katika sura hii kutambua mabadiliko ya vokali za nomino mkopo za Kiturkana. Kanuni za Sandhi zitatumika kueleza motisha ya kujiri kwa badiliko ya irabu kama badiliko hili la vokali ni kwa sababu ya kupata silabi mahususi au la.

Vokali za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili husawiri mabadiliko mbalimbali za kimofofonolojia zinapoingizwa katika Kiturkana. Katika kazi yetu tumebaina mifanyiko ya kimofofonolojia zifuatazo ambazo vokali za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hupitia kabla ya kukubalika katika mfumo wa Kiturkana.

## 4.1 Udondoshaji wa vokali

Schane (1973) anasema kwamba kudondoshwa kwa vokali ni mojawapo wa sheria asilia ambazo zinahusu kanuni za muundo mwafaka wa silabi. Udondoshaji wa vokali za nomino mkopo za Kiturkana hutokea katika mazingira ya vokali kutanguliwa na konsonanti. Ifuatayo ni mifano ya udondoshaji ni kama ifuatavyo:

/Kitabu / > [akitab+u] > [akitab]

Katika mfano huu vokali /u/ katika nomino ya Kiswahili inadondoshwa katika silabi **bu** kisha tunapata silabi funge ya Kiturkana yaani **tab.** Badiliko hili linamotishwa kifonolojia kwani kusudi lake ni kupata muundo mwafaka wa silabi ya Kiturkana ambao

ni funge yaani KIK. Nomino kitabu ina silabi tatu yenye muundo wa konsonanti irabu (KI) yaani / ki + ta + bu/

KI + KI + KI

Vokali /u/ ndio ilikuwa ikuzua silabi /bu/ na mkazo ulikuwa katika silabi ya pili kutoka nyuma yaani silabi **ta; ki'tabu** ili kudumisha mkazo huo katika Kiturkana silabi **ki** ambayo inatiwa mkazo. Udondoshaji wa vokali /u/ ni kusahilishaji matamshi kwa kuepuka uziada. Hii ni kwa sababu ni vigumu kutamka [akitabu] kwani shadda ikiwa katika silabi **ta** utamkaji utakuwa mgumu.

### 4.1.1 Udondoshaji wa vokali /i/

Baadhi ya nomino nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili zilizo na vokali /i/ katika silabi ya mwisho, vokali /i/ inadondoshwa :

/kazi/ > [ ɛ-kasi] > [ɛkas] kazi

Nomino [kazi ] inapokopwa na Kiturkana, hupitia mageuzi ya kifonolojia kama vile kuimarika kwa kikwamizwa kilicho ghuna /z/ na kuwa kikwamizwa /s/ inayohitaji nguvu nyingi kutamka. Inakuwa vigumu mno kutamka /ɛ-ka –si/ ilivyo na idadi ya silabi. Ili kusahilisha utamkaji vokali /i/ hudondoshwa na ili kupata silabi funge inayoundwa kwa konsonanti irabu konsonanti kwa hivyo *kas* ina kuwa silabi funge na nomino yenye inakuwa na idadi ya silabi mbili yaani /ɛ-kas/ /I$KIK/

Mifano nyingine ya nomino mkopo ambazo vokali /i/ inadondoshwa ili kupata silabi funge na kuwa na idadi ya silabi mbili ni:

/basi/ > /a- ba-si/ > [abas] basi

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| /kadi/ | > | /a-ka-di/ | > | [akad] | kadi |
| /kabati/ | > | /a-ka-ba- ti/ | > | [akabat] | kabati |
| /ɳazi/ | > | /a- ɳa-si/ | > | [angas] | kazi |

Tunaweza kubuni kanuni ifuatayo kuelezea udondoshaji huu:

Kanuni : [i] > K / -/i/

[i] > [ b, z, s, t] / - /i/

Kanuni hii ina maana kwamba vokali /i/ inadondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na konsonanti /b/, /s/, /z/ na /t/ katika silabi ya mwisho ya nomino ya Kiswahili. Nomino hizi mkopo za Kiturkana zimedondosha vokali /i/ ili kupata silabi mbili itakuwa rahisi kutamka hivyo basi kuepuka uziada. Hii ni kwa sababu katika utamkaji wa maneno ya Kiturkana iwapo neno linafaa kutamkwa kwa haraka vokali /i/ hudondoshwa.

Hata hivyo kuna baadhi ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili ambazo zinadondosha vokali katika silabi ya mwisho ya nomino hizo za Kiswahili kisha kunachopeka vokali ya chini katika mifano ni kama ifuatavyo:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| /gari/ | > | /a- ga:r/ | > | [aga:r] | gari |
| /meli/ | > | /a-mɛ:l/ | > | [amɛ:l] | meli |

Nomino hizi mbili za Kiswahili gari na meli inapoingizwa katika Kiturkana irabu ya silabi ya mwanzo inarefushwa na irabu /i/ ya silabi ya mwisho kudondoshwa na matokeo ni kwamba neno linakuwa silabi tatu kama ifuatavyo:

| Nomino | | muundo wa silabi | Maana |
|---|---|---|---|
| i) | /a-ga-:r/ | I$KI$IK | Gari |
| ii) | /amɛ:l/ | I$KI$IK | Meli |

Tunaweza kubuni kanuni hii kuelezea udondoshaji wa vokali / i/ kwenye nomino hizi mbili za Kiswahili yaani gari na meli.

[i] > K / -I

$$[I] > \begin{Bmatrix} l \\ r \end{Bmatrix} / - [i]$$

Kanuni hii inaeleza kwamba vokali /i/ inadondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na kitambaza au kimadende.

Ni bayana kwamba udondoshaji ni mageuzi ya kifonolojia ambayo kusudi lake ni kupata muundo mwafaka wa silabi ya lugha husika mathalan katika nomino mkopo za Kiturkana ambapo vokali /i/ imedondoshwa ili kupata muundo wa silabi funge yaani **KIK.**

## 4.2 Uchopekaji wa vokali

Uchopekaji ni mchakato wa kifonolojia ambao unahusu sauti kuchopekwa au kuongezwa kwenye nomino mkopo. Uchopekaji wa irabu katika Kiturkana ni mchakato ambao unamotishwa kimofofonolojia kama kanuni ya mofolojia ya ‘MP’ katika nadharia ya fonolojia zalishi awali (NFZA)

Uchopekaji wa vokali ndio mchakato wa kifonolojia ambao umeshamiri katika lugha ya Kiturkana. Lengo la mchakato wa uchopekaji wa vokali katika nomino mkopo za Kiturkana ni wa kupata muundo wa silabi husika katika Kiturkana hususan muundo ulio wazi. Uchopekaji wa vokali katika Kiturkana unaweza kutokea mwanzoni wa konsonanti ya nomino mkopo, katikati au mwishoni. Tunaweza kusawiri uchopekaji wa vokali katika nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Uchopekaji wa vokali /a/

Vokali /a/ ambayo ni ya mbele, chini ya ulimi na isiyo mviringo huchopekwa kwenye nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili. Uchopekaji ambao umeshamiri sana ni ule wa unatokea mwanzoni wa nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili. Kusudi kuu la uchopekaji huu ni kupata muundo wa silabi ya irabu pekee. Vokali hii husahilisha utamkaji wa nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Mifano ya uchopekaji wa vokali /a/ ni kama ifuatavyo:

| Kiturkana | | Kiswahili | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| /barua / | > | /a+ barua/ | > | [abarua] | barua |
| /gari/ | > | / a+ ga:ri/ | > | [aga:r] | gari |
| lɛsɔ/ | > | /a+lɛsɔ/ | > | [alɛsɔ] | leso |
| /sinɛma/ | > | /a+sinɛma/ | > | [asinma] | sinema |

Katika mifano hii, tunaona kwamba vokali /a/ ambayo ni vokali ya mbele chini isiyo mviringo inachopekwa mwanzoni mwa nomino mkopo za Kiturkana kutoka kwa

Kiswahili ili kupata silabi ya irabu pekee. Pia vokali /a/ huwasilisha mofimu ya jinsia ya kike katika nomino za Kiturkana.

Hata hivyo nomino ya Kiswahili, gari inapokopwa na Kiturkana inachopekwa vokali /a/ mwanzoni na baada ya konsonanti /g/. Uchopekaji wa vokali /a/ mwanzoni hukusudiwa kupata mofimu ya jinsia ya kike na kwa wakati huo huo kupata silabi ya irabu pekee ambayo husahilisha utamkaji wa nomino mkopo husika. Nayo vokali /a/ inayochopekwa baada ya konsonanti /g/ dhima yake ni kupata silabi yenye muundo wa Konsonanti Irabu (KI).

### 4.2.2 Uchopekaji wa vokali /ɛ/

Baadhi ya nomino za Kiswahili zinapokopwa na Kiturkana huchopekwa vokali mwanzoni mwao ili kupata muundo wa silabi ya irabu pekee ya Kiturkana. Uchopekaji huu husahilisha utamkaji wa nomino mkopo hizi za Kiturkana kutoka kwa Kiswahili. Tunaweza kusema mageuzi ya vokali ya nomino Kiswahili yanapoingizwa katika Kiturkana yanamotishwa kifonolojia kama anavyodai Schane(1973) kwamba kuna umuhimu wa kuzingatia ruwaza ya mifanyiko yoyote ile ya kifonolojia hususan ile ya asilia, Kwa hivyo uchopekaji wa vokali /a/ ni kupata silabi ya irabu pekee. Mifano ya nomino mkopo zilizochopekwa vokali /ɛ/ mwanzoni kama ifuatavyo:

| **Kiswahili** | | | | **Kiturkana** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|---|---|
| /msalaba/ | > | / ɛ+musalaba/ | > | [ ɛmusalab] | msabibu |
| /paka/ | > | /ɛ+paka/ | > | [ ɛpaka] | paka |
| /bɛi/ | > | /ɛ+bɛi/ | > | [ɛbɛi] | bei |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| /sabuni/ | > | /ɛ+sabuni/ | > | [ɛsabuni] | sabuni |
| /jikɔ/ | > | /ɛ+jikɔ/ | > | [ɛjikɔ] | jiko |
| /gunia/ | > | /ɛ+gunia/ | > | [ɛgunia] | gunia |
| /kahawa/ | > | /ɛ+kawa/ | > | [ɛkawa] | kahawa |

Kutokana na mifano hii ni bayana kwamba vokali /ɛ/ huchopekwa mwanzoni mwa nomino za Kiswahili zinapokopwa na Kiturkana ili kupata silabi ya irabu pekee. Silabi hii yenye muundo wa irabu pekee huwa mwanzoni mwa nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Aidha, uchopekaji wa vokali /ɛ/ mwanzoni mwa nomino mkopo za Kiturkana hulenga kupata mofimu ya jinsia ya kiume hivi basi kuainisha nomino mkopo za Kiturkana husika katika jinsia ya kiume.

### 4.2.3 Uchopekaji wa vokali /u/

Vokali /u/ huchopekwa kwenye baadhi ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili ili kuvunja silabi ya konsonanti ya pekee inayoundwa na nazali /m/. Sababu ni kwamba hamna silabi ya konsonanti pekee inayoundwa na nazali /m/ katika Kiturkana. Silabi ya konsonanti ya nazali /m/ inayochopekwa vokali /u/ ni ile ya mwanzoni mwa nomino ya Kiswahili na sio silabi ya mwisho. Mifano ya nomino mkopo za Kiturkana zinazosawiri mifanyiko hii ni kama ifuatavyo:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| /mkate/ | > | /a+ m+u +gati/ | > | [amugati] |
| / msalaba / | > | /ɛ+mu+sa+la+ba/ | > | [ɛmusalaba] |
| /msikiti/ | > | /ɛ+m+u+sikiti/ | > | [ɛmusikiti] |
| /mʧɛlɛ/ | > | /ɛ+m+u+culɛ / | > | [ ɛmucɛlɛ] |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| /mzuɳu/ | > | /ɛ m+ u+ɳut/ | > | [ɛmuɳut] |
| /mtarɔ/ | > | /a+m+u+tarɔ/ | > | [amutarɔ] |
| /mɳɔrɔrɔ/ | > | / a+m+uɳɔrɔrɔ/ | > | [amuɳɔrɔrɔ] |
| /mʃahara/ | > | /ɛ+m+u+sara/ | > | [ɛmusara] |

Mifano hii tuliyotoa inaonyesha kwamba uchopekaji wa vokali /u/ unatokea katika mazingira ya kutanguliwa na konsonanti /m/ ambayo ni nazali inayotamkwa mdomoni na iliyo ghuna. Nazali /m/ hii huwa ni silabi ya konsonanti pekee katika Kiswahili na ili kupata silabi yenye muundo wa konsonanti irabu (KI) yaani <u>**mu**</u> katika Kiturkana vokali /u/ inachopekwa. Kwa hivyo uchopekaji huu unamotishwa kifonolojia.

### 4.2.4 Uchopekaji wa vokali /i/

Uchopekaji wa vokali /i/ ni mfanyiko mwingine wa kimofofonolojia unaopitiwa na baadhi ya nomino ya Kiswahili inayoingizwa katika Kiturkana. Nomino mkopo ya Kiturkana kutoka Kiswahili inayosawiri uchopekaji wa vokali /i/ ni kama ifuatayo:

/mtihani/ > / ɛ+m+i+tian/ > [ ɛmitian] mtihani

Mfano huu unaonyesha kwamba vokali /i/ inachopekwa baada ya nazali m/ ambayo ni silabi yenye muundo wa konsonanti pekee katika nomino ya Kiswahili [mtihani]. Katika mchakato huu wa uchopekaji wa vokali /i/ baada ya nazali /m/ inatupa silabi yenye muundo wa Konsonanti Irabu **KI** yaani **mi** kama ilivyo katika nomino mkopo ya Kiturkana *emitiani*.

Kuna uchopekaji wa vokali /i/ mwishoni silabi ya nomino mkopo. Kwa mfano:

/ɲanɔ/ > /aɲakanɔ+i/ > [aɲakanoi]

Katika mfano huu tunaona kwamba vokali /i/ ambayo ni vokali ya mbele juu inapachikwa baada ya vokali /ɔ/ ili kupata muundo wa silabi ya vokali pekee.

Uchopekaji wa vokali katika nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili ni mchakato wa kifonolojia ambao kusudi lake ni kupata silabi ya Kiturkana yaani silabi ya irabu pekee inayotokea mwanzoni mwa nomino mkopo za Kiturkana wakati ambapo vokali /a/ au / ɛ/ inachopekwa katika nomino za Kiswahili zinazoingizwa katika Kiturkana. Aidha , uchopekaji wa vokali /u/ au /i/ baada ya konsonanti ya nazali /m/ ambayo huwa silabi ya konsonanti pekee, kusudi lake ni kupata silabi yenye muundo wa konsonanti irabu **KI.**

Ni bayana kwamba uchopekaji wa vokali kama mchakato wa kimofofonolojia unatekeleza jukumu la kugeuza nomino za Kiswahili zikubalike katika fonolojia ya Kiturkana.

## 4.3 Uyeyushaji

Mabadiliko mengine ambayo vokali za nomino za Kiswahili hupitia wakati ambapo zinaingizwa katika Kiturkana ni uyeyushaji. Lengo la uyeyushaji katika Kiturkana ni kupata muundo mwafaka wa silabi ya nusu irabu irabu. Na kama anavyosema (Schane (1973) kwamba sababu mojawapo ya kuunda nusu irabu ni kuleta muundo mwafaka wa silabi. viyeyusho au nusu irabu huundwa wakati ambapo irabu /u/ huimarika na kuwa nusu irabu /w/ na /i/ nusu irabu /j/. Kwa kawaida vokali huhitaji nguvu kidogo

kuzitamka zikilinganishwa na nusu –irabu. Hii ndio sababu ya madai kwamba vokali imeimarika na kuwa nusu irabu.

Naye Anderson (1972) anasema kwamba uyeyushaji unaweza kutokea wakati ambapo /u/ inafuatwa na [+irabu, -juu]. Haya mawazo ya Anderson yanawiana na ya Schane kwamba mchakato huu huhusisha vokali /i/ na /u/ ambazo hugeuka na kuwa viyeyusho /j/ na /w/ kama inavyojitokeza katika nomino mkopo za Kiturkana zifuatazo:

/w ɛmb ɛ / > /ɛ+u+ɛmb/ > [ɛwɛmbɛ]

Tunaweza kubuni kanuni hii :

/u/ > /w/ / /ɛ/

Hapo tunaona kwamba vokali /u/ ya nyuma inapotangulia vokali /ɛ/ ambayo ni mbele nusujuu zinaungana na kuunda /w/

Mfano wa nomino mkopo ya Kiturkana inayosawiri uyeyushaji wa vokali zake kuwa /w/ ni kama ifuatavyo:

/ winɔ / > ɛ+ u+i+nɔ/ > [ɛwinɔ]

Sheria inayoelezea mchakato huu wa uyeyushaji wa vokali za nomino za Kiswahili zinazoingia katika Kiturkana ni:

/u/ > /w/ / I (isiyo /u/ )

/u/ > /w/ / /i/

Kwa hivyo katika nomino wembe na wino zinapoingizwa katika Kiturkana tunaona kwamba vokali /u/ inaungana na vokali /i/ kuunda nusu irabu /w/.

Mifano ya nomino mkopo za Kiturkana ambapo vokali /i/ inabadilika na kuwa nusu vokali /j/ katika mazingira ya kutangulia vokali isiyo /i/yenyewe na wakati huo huo vokali /u /yake

/waja/ > /a+u+a+i+a/ > [ awaja]

Vokali za nomino mkopo ya Kiturkana **awaya** imetupia uyeyushaji wote yaani ya / i/ kugeuka kiyeyusho /j/ katika mazingira ya kutangulia vokali isiyo /i/ kwa upande na kwa upande mwingine u inabadilika na kuwa /w/ katika mazingira ya kutangulia vokali isiyo /u/ wakati iliingizwa . Japo nomino **waja** imekopwa na Kiswahili kutoka Kiingereza, Kiturkana kimekopa nomino **waja** kutoka kwa Kiswahili kulingana na Kamusi ya Kiingereza – Kiturkana, ndio maana tukaainisha nomimo **waja** kwenye mchakato huu. Isitoshe tulieleza katika utangulizi wa kazi hii kwamba hatutajikita katika kutazama iwapo Kiswahili kilikopa nomino husika kutoka lugha nyingine.

pia vokali /ɔ/ huungana na vokali /a/ na kuunda kiyeyusho /w/ kwa mfano:

/s ɔ ma / > / aswɔm ɛ t/

/s ɔ ma/ > / ɛswɔm ɛ /

Baadhi ya nomino mkopo ambazo zinasawiri uyeyushaji wa vokali /i/ kuwa j/ katika mazingira ya kutangulia vokali /i/ ni wingi wa nomino mkopo zilizokopwa na Kiturkana kutoka Kiswahili. Kwa mfano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ŋidis+**i**+ɔn/ | > | [ ŋidisjɔn] | wingi wa ndizi |
| /ŋikabut+i+ɔ/ | > | [ŋikabutjɔ/ | makabuti |
| /ŋaga:r+**i**+ɔ/ | > | [ŋaga:ryɔ] | magari |

Tunaweza kubuni sheria ifutayo kuelezea mabadiliko ya vokali za nomino mkopo za Kiturkana kama tulivyoainisha hapo juu.

i/ > /j/ / - / ɔ/

Hapo tunaona kwamba vokali /i/ ambayo ni ya mbele juu inatangulia vokali /ɔ/ ambayo ni nyuma nusu chini, zinaunda nusu irabu /j/.

Mifano nyingine ya uyeyushaji wa nomino mkopo za Kiturkana ni kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| /ŋakaratas+i+a/ > | [ ŋakaratasja] | karatasi |
| /ŋakad+i+a/ > | [ŋakadja] | kadi |
| /ŋabas+i+a/ > | [ŋabasya] | mabasi |

Tunaweza kueleza mabadiliko ya haya vokali za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili kwa kanuni ifuatayo:

Kanuni : / i/ > /j/ / /a/

Hii ina maana kwamba katika mazingira ambayo vokali /i/ ambayo ni ya mbele na juu inatangulia vokali /a/ ambayo chini basi zinaungana na kuunda nusu irabu /j/

Uyeyushaji katika vokali za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili ni kupata silabi ya nusu irabu irabu ambayo husahilisha utamkaji wa nomino hizi mkopo katika Kiturkana.

### 4. 3. 1 Ubadala wa vokali

Kuna nomino za Kiswahili zinapoingizwa katika Kiturkana vokali zao zinabadilishwa na za Kiturkana. Hii ni kwa sababu mfumo wa vokali za Kiturkana ni tofauti na za Kiswahili. Ubadilishaji wa vokali unasawiriwa kwenye baadhi ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili kama ifuatavyo:

/mkatɛ/ > [amugat**i**]

Katika nomino ya Kiswahili */mkatɛ/* inapoingizwa katika Kiturkana vokali /ɛ/ ambayo ni mbele nusujuu inabadilika na kuwa vokali /i/ anbayo ni ya mbele na juu katika Kiturkana.

Kanuni : /ɛ/ > [i]

Mfano mwingine wa ubadala wa vokali ni pale ambapo nomino ya Kiswahili, *Hoteli* inapoingizwa katika Kiturkana inakuwa eotel. Yaani:

/hɔtɛli/ > [**ɛɔ**tel]

Kanuni : ɔ > [ɛɔ]

Kanuni hii ina maana kwamba vokali /ɔ/ ya Kiswahili inabadilishwa na vokali /ɛɔ/ katika Kiturkana

Ubadala wa vokali /a/ ya Kiswahili kuwa /a:/ ya Kiturkana kwa mfano katika nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili .

Mifano

| **Kiswahili** | | **Kiturkana** |
|---|---|---|
| /g**a**ri/ | > | [g**a:**r] |
| /kazi/ | > | [ɛkaz] |
| /b**a**hasha/ | > | [ ab**a:**ca] |

kanuni : /a/ > [a:]

vokali ya /a/ nomino ya Kiswahili inabadilishwa na ya vokali ya /a:/ ya Kiturkana.

**Ubadala wa vokali /ɛ/ na kuwa /ɛ:/**

Nomino ya Kiswahili *meli* inapoingizwa katika Kiturkana vokali yake /ɛ/ hubadilishwa na vokali ya / ɛ:/.

/mɛli/ > [mɛ:l]

Kanuni : /ɛ/ > [ɛ:]

Vokali ya Kiswahili /ɛ/ ni vokali ya mbele na nusujuu inabadilika na kuwa vokali /ɛ:/ ya Kiturkana ambayo ni vokali ya mbele lakini nusu chini.

Ubadala mwingine wa vokali ni ule ambapo vokali ya Kiswahili /u/ inabadilishwa na kuwa vokali /ɔ/ ya Kiturkana kwa mfano:

| **Kiswahili** | | **Kiturkana** |
|---|---|---|
| /m**u**hɔgɔ/ | > | [ɛmɔgɔ] |
| /maʧaraupu/ | > | [aɳamasurupɔ] |
| /simu/ | > | [ɳasimɔn] |
| /mwalimu/ | > | [ɛmalimɔt] |
| /sukariguru/ | > | [ɳisikaraɳururyɔ] |

Kanuni : / u / > [ɔ]

Kanuni hii inaeleza kwamba wakati nomino ya Kiswahili *muhogo* inakopwa na Kiturkana inakuwa *emogo* ambapo vokali ya Kiswahili /u/ ambayo ni vokali ya nyuma na juu inabadilika na kuwa vokali /ɔ/ ambayo ni nyuma na nusu -juu.

Ubadala wa vokali /a/ ya Kiswahili na kuwa ya Kiturkana /i/

Vokali / ɔ / ya nomino ya Kiswahili */sɔmɔ/* inabadilika na kuwa /ɛ/ kuwa ya nomino mkopo ya Kiturkana yaani /asɔmɛt/ inapoingizwa katika Kiturkana.

*/sɔmɔ/* > /asɔmɛt/

Tunaweza kubuni kanuni hii: /ɔ/ > /ɛ/

Kanuni ina maana kuwa nafasi ya vokali /ɔ/ ambayo ni vokali ya nyuma na nusu-juu katika nomino ya Kiswahili *somo* inachukuliwa na vokali /ɛ/ ya mbele nusu-juu katika

nomino mkopo *asomet*. Ubadilishaji huu unarahisisha utamkaji wa nomino *somo* inapoingizwa katika Kiturkana.

Hatimaye kuna ubadala wa vokali /i/ ya nomino Kiswahili ambayo hubadilika na kuwa /u/ inapokopwa na Kiturkana. Kwa mfano:

/sikukuu/ > / ɛsukukuu/

### 4.3.2 Uwiano wa vokali

Uwiano wa vokali kulingana na Scheme (1973) ni kwamba vokali huweza kukubaliana kwa hali ya urefu, hali ya kuwa mbele au nyuma na mkao wa mviringo na vokali nyingine namna inayotokea katika mfanyiko wa uwiano wa vokali.Uwiano wa vokali ni mojawapo wa kanuni na uwiano wa vipashio vinavyoathiriana kisifa lakini kwa mbali. Badiliko lingine linakumba vokali za nomino mkopo ya Kiturkana kutoka kwa Kiswahili ni uwiano wa vokali. Kwa mfano:

/mkristɔ/ > [ɛkristɔ**it**]

Katika mfano huu tunaona kwamba vokali /ɔ/ ya nomino ya Kiswahili *mkristo* inawiana vokali /i/ wakati inaingizwa katika Kiturkana na kuwa /ɔi/ katika nomino mkopo *ekristoit.*

Nomino nyingine ya Kiswahili ambayo inakumbwa na uwiano wa vokali ni /bɛi/ ambapo katika Kiturkana inakuwa /ɛbɛ**i**./. Katika uwiano huu vokali /ɛ/ ambayo ni vokali ya chini inawiana na vokali/ i/ ya juu.

Uwiano mwingine katika nomino mkopo /ɛmal**ai**kat/ na /p**ai**p**ai**/ambapo kuna uwiano kwa vokali mbili ambayo ni /a/ ambayo ni vokali ya chini na / i/ ambayo ni vokali ya juu. Uwiano wa vokali ni mchakato wa kimofofonolojia kwani inahusu mofolojia kama anasema Iribemwangi (2008) katika tasnifu yake ya uzamivu kwamba ni mchakato unayohusu kwa kiwango kikubwa masuala ya kimofofonolojia na kwa kiasi kidogo ya kifonolojia. Iribemwangi akimdara Kenstonicz (1994), kwamba ni hali ya kifonolojia ambapo vokali katika hali fulani huwiana kupata sifa fulani.

Uwiano wa vokali katika Kiturkana unahusu nomino mkopo tofauti na lugha ya Kiswahili ambapo uwiano wa vokali huhusu unyambuzi wa vitenzi. Kusudi la mchakato huu katika Kiturkana ni kupata muundo wa silabi ya irabu pekee . Tunaweza kusema kwamba mchakato huu ni wa kimofofonolojia.

**Hitimisho**

Katika sura hii tumeshughulikia mabadiliko ya vokali ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Tumeweza kubaini kwamba kuna baadhi ya vokali za nomino za Kiswahili zinazodondoshwa wakati zinaingia katika mfumo wa fonolojia ya Kiturkana. Kusudi la udondoshaji wa vokali hizi za nomino mkopo ni kupata muundo mwafaka wa silabi.

Mabadiliko mengine tuliyobaini katika sura ni uchopekaji wa vokali katika nomino za Kiswahili zinapoingizwa katika Kiturkana. Katika uchopekaji tukatambua kwamba kuna uchopekaji wa mwanzoni wa nomino mkopo ili kupata muundo wa silabi ya irabu pekee. Uchopekaji wa mwanzoni wa vokali ni vokali /a/ au /ɛ/ . uchopekaji mwingine ni ule

katika konsonanti ili kupata muundo wa silabi ya KI. Vokali zinazochopekwa ili kuvunja mfuatano wa konsonanti ni /u/ na /i/. Hata hivyo uchopekaji wa vokali /u/ ni unaonekana ni mchakato ambao ni kinyume cha udondoshaji wa Kiswahili kwani katika Kiswahili vokali /u/ udondoshaji katika hali ya nazali /m/ kutangulia vokali /u/ ili kupokeza nazali /m/ sifa za usilabi.

Pia tuligundua kwamba vokali ya nomino mkopo za Kiturkana ni ubadilishaji ambapo baadhi ya vokali zinabadilishana wakati ambapo nomino ya Kiswahili inakopwa na kuingizwa katika Kiturkana.

Aidha, uyeyushaji wa vokali umekumba baadhi ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hususan zinapoandikwa katika hali ya wingi.

Hatimaye uwiano wa vokali ni mchakato mwingine wa kimofofonolojia ambayo vokali ya nomino mkopo za Kiturkana zimepitia.

## SURA YA TANO

# 5.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 5.1 Utangulizi

Uchunguzi wetu ulikusudia kuchanganua na kutathmini mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Katika uchunguzi wetu tulielekezwa na nadharia ya fonolojia zalishi asilia (NFZA) ambayo imetuwezesha kuelewa muundo ndani na muundo nje wa nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili kupitia kanuni za uasilia. Kupitia kanuni ya uasilia tumeeleza mifanyiko ya kimofofonolojia ambayo nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili zimepitia ndipo zikakubalike katika mfumo wa fonolojia ya Kiturkana.

Katika sura hii tutatoa muhtasari wa kazi yetu, hitimisho na mapendekezo ambayo yatashughulikiwa na tafiti za siku za usoni ambayo kazi yetu haikuweza kudara.

### 5.1.1 Vipengele vya fonolojia ya Kiturkana

Utafiti wetu ulilenga kuchanganua mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Utafiti huu umeyakinisha haipothesia tuliyoanisha. Tulidai kwamba fonimu za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili zina uhusiano wa moja kwa moja na fonolojia ya Kiswahili na Kiturkana. Kazi yetu imebaini kwamba kuna fonimu ambazo zipo katika Kiswahili lakini hazipo katika Kiturkana kwa hivyo nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili inapoingizwa katika Kiswahili ni lazima mabadiliko ya kifonolojia yajiri ndipo nomino hizo mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili ziafike mfumo wa fonolojia ya Kiturkana. Vile vile tulibaini kwamba miundo mingi ya silabi zilizo katika Kiswahili zipo katika Kiturkana.

### 5.1.2 Mabadiliko ya kifonolojia ya konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana

Utafiti wetu umebaini kwamba konsonanti za nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hupitia mabadiliko ya kifonolojia kama vile udhoofikaji wa konsonanti, uimarikaji wa konsonanti, udondoshaji wa konsonanti, uchopekaji wa konsonanti, usilimisho pamwe nazali na ubadala wa konsonanti ili nomino hizi za Kiswahili zikubalike katika Kiturkana kwa kusahilisha utamkaji, kupata muundo mwafaka wa silabi na mofimu ya jinsia ambayo hutumiwa kuainisha nomino za Kiturkana.

### 5.1.3 Mabadiliko ya kifonolojia ya vokali za nomino mkopo za Kiturkana

Kazi yetu imebaini kwamba vokali za nomino za Kiswahili zinazokopwa na Kiturkana hupitia mabadiliko ya kifonolojia kama vile udondoshaji wa vokali, uchopekaji wa vokali, ubadala wa vokali, uyeyushaji na uwiano wa vokali ili nomino hizi za Kiswahili zikubalike katika Kiturkana. Kukubalike huku kumewezasha upatanikaji wa miundo wa silabi, usahilishaji wa utamkaji na upatanikaji wa mofimu ya nomino husika ambapo huianishwa katika jinsia ya kiume au kike.

## 5.2 Muhtasari wa utafiti

Utafiti wetu umeonyesha mabadiliko ya kimofofonolojia ambayo nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili hupitia zinapoingizwa katika Kiturkana. Kazi hii ni muhimu kwani ndio ya kwanza kushughulikia mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili.

Mbinu ya utafiti tuliyotumia kukusanya data yetu ni utafiti wa maktabani ambapo tulichota data yetu kutoka kwa Bibilia ya Kiturkana, Misali ya Kiturkana na Kamusi ya Kiingereza — Kiturkana. Data tulikusanya kutoka maktabani imewasilishwa kifonetiki na kiothografia.

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti wetu umeshughulikia uchanganuzi wa kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili. Watafiti wengine wanaweza kushughulikia maneno mkopo mengine katika Kiturkana kutoka Kiingereza, Kipokot, Kirendile, Kimerile na Kikaramojok.

Waaidha, tulitumia nadharia ya fonolojia zalishi asilia katika uchanganuzi wetu. Watafiti wengine wanaweza kutumia nadharia ya vipande sauti kuchanganua mifanyiko ya kimofofonolojia ya nomino mkopo za Kiturkana.

Hatimaye tafiti nyingine za baadaye zinaweza kushughulikia mabadiliko ya kimofofonolojia kwa kudara elementi kama vile toni, mkazo na kiimbo ya nomino mkopo za Kiturkana ambayo utafiti wetu haukushughulikia.

## MAREJELEO


Anderson, J.M. (1975) *Structural Aspects of Language Change*. London: Longman.

Antila R. (1972) *An Introduction to Historical and Comparative Lingunstics*. New York: Maclmillan.

Apel , R. and Muyken P. (1987) *Language contact and Lingualism*. London: Edward Arnold

Bakari. M. (1982). *The Mophonology of the Kenyan Swahili Dialect. PhD Thesis.* University of Nairobi.

Ball, M. (1971) *Prestige Languages and word- borrowing*: *The changing status of Arabic and English in Kenya*. Studies in African Linguistics, 131-137.

Barret, A. ( 1990), Turkana English Dictionary. London: Macmillan Education Ltd.

Bynon T.(1977). *Historical Linguistics*. London Macmillan.

Chomsky, N. and M. Halle (2005). *Language Borrowing Diffusion*: An Overview in Intercultural Communication Studies. X1:4200

Chikanza, J. (1986). 'Borrowing in Shona" Unpublshed MA Dissertation. Florida University of Florida

Chimhundu, H.V. (1983). "Adaptation in Shona" Unpublished D. Phil Thesis. Harare.

Dimmendaal, Gerrit Jan. 1983. *The Turkana language*. Cinnaminson: Foris Publications.

Dimmendaal, Gerrit Jan. 1993. *Review of Turkana-English Dictionary by A. Barrett.Research in African Literatures* Vol. 24, No. 2, Special Issue on Oral Literature (Summer, 1993), pp.131-133.

Dohlus, K. (2005). Phonetics or phonology: Asymmetries in loanword adaptations–French and German mid front rounded vowels in Japanese. *ZAS Papers in Linguistics*, *42*, 117–13.

Evans, W. M. (2014). *Mophophonological changes of borrowed words from English to Lubukusu dialect of Western Kenya.* International Journal of English and Literature, 5(2), 45–51.

Friesner, M. L. (2009). *The social and linguistic predictors of the outcomes of borrowing in the speech community of Montreal.* Citeseer. Retrieved from http://citeseerx.ist.psu.edu/viewdoc/download?doi=10.1.1.226.380&rep=rep1&t

Guthrie, M. (1967). The classification of Bantu Languages. London: Dawsons of Pall Mall.

Habwe, Matei na Nyonje, ( 2010) *Darubini ya Isimujamii kwa shule na vyuo*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Hockett, C. F. (1958). A course in modern linguistics. *Language Learning*, *8*(3-4), 73–75.

Hock, H. H. (1991). *Principles of historical linguistics*. Walter de Gruyter. Retrieved from https://books.google.com/books?

Holden, K. (1976). Assimilation rates of borrowings and phonological productivity. *Language*, Volume 15, 131–147.

Hooper, J. B. (1976). *An introduction to natural generative phonology*. Academic Press.

Houpe, D. W. (1978). *Loanwords in Baraza: a study of lexical origins in a Swahili language newspaper*. University of North Carolina at Chapel Hill.

Hyman, L. M. (1970). *Phonology, Theory and Analysis*. San Francisco: Rinehart and Winston.

Iribemwangi, P.I. (2008) A Synchronic Morphophonology of Standard Kiswahili. Unpublished PhD Thesis, University of Nairobi.

Iribemwangi, P. I. (2012). Phonology of Borrowed Lexicon in Standard Kiswahili. In *Reyono Journal of Interdisciplinary Studies.* St. Thomas College, Kozhencherry, India. Vol. 1 No. 2. pp 59-74.

Iribemwangi, P.I (2013). Cultural Transfer from Europe and Asia to Africa: Evidence from Borrowed Lexicon Adapted into Kiswahili. *International Journal of Education and Research.* Vol. 1 No. 8. pp 1-14.

Iribemwangi na Mukhwana (2011) Isimujamii, Nairobi: Focus Publishers.

Johannes, S. (1872). The Relationship of Indo-Germanic Languages. Germany: University of Bonn Press.

Kadenge, M., na Mabugu, P. (2009). The phonological characteristics of Shona loanwords from English. *Nawa (Windhoek, Namibia)*, *3*(1), 101–116.

Kang, Y. (2008). English/z/in 1930s Korean. Retrieved from http://individual.utoronto.ca/yjkang/files/ICEAL2008handout.pdf 128

Kang, Y. (2010). Tutorial overview: Suprasegmental adaptation in loanwords. *Lingua*, *120*(9) 2295– 2310.

Katamba, F. (1992) *An Introduction to Phonology.* Longman: London.

Kihore, Y. M. Massamba, D and Matangila, M. (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Kunene, D. P. (1963). Southern Sotho words of English and Afrikaans origin. *Word-Journal of the International Linguistic Association*, *19*(3), 347–375.

Lass, R. (1984) Phonology : An introduction to basic concepts. Cambridge: Cambridge University Press.

Lyons, J. (1968). *Introduction to Theoretical Linguistics*. New York: Cambridge University Press.

Leiden (1983) *The Turkana Launguage.* Netherlands: Foris Publications Holland.

Massamba, D. P. (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam. TUKI.

Massamba, D. P. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha:* Dar-es-Salaam. TUKI.

Mbaabu, L. (1996). *Language Policy in East Africa: A Dependancy Theory Perspective.* Nairobi; General Printers Ltd.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi; Longhorn Publishers.

Mohammed, M. A.(2001). Modern Swahili Grammar. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Mugenda, O. and Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative approaches*. Nairobi: Acts Press.

Muhati, P. (2000). Matatizo ya Kuelewana Kimaongezi miongoni mwa Wabaluhyia wa Magharibi mwa Kenya Wanaozungumza Lahaja za Kiisukha, Kikisa, Kiloogoli na Kibukusu.Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mulwa, M. (2014), *Fonolojia ya nomino – mkopo za Kikamba kutoka Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili chuo kikuu cha Nairobi : Nairobi.

Mutisya, J. (1986). Concordial Agreement in Kiswahili and Kikamba, Unpublished PhD Thesis,University of Nairobi.

Mwaliwa, H. (2000) Ulinganishi wa mofofonolojia ya Kiswahili na Kidawida. Tasnifu ya uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mwihaki, A. N. (1998). Loanword Nativisation: A Generative View of the Phonological Adaptation of Gikuyu Loanwords, Doctoral Thesis, Kenyatta University.

Mwita, L. C. (2009). The Adaptation of Swahili Loanwords from Arabic: A Constraint-Based Analysis. In *the Journal of Pan African Studies,* Vol. 2 *No. 8, 46-60*

Newman, P. (2000). Comparative Linguistics in *D. Nurse and B. Heine (eds) African Languages: An Introduction:* Cambridge University Press

Njeru, M. D. W. (1990). Lexical Expansion in Kiswahili: A Study of Strategies in Corpus Development. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ngowa, N. (2015), Uchanganuzi wa nomino-mkopo za Kigiriama kutoka Kiingereza.Tasnifu ya uzamifu chuo kikuu cha Nairobi.

Owino, D. (2003). *Phonological nativation of Dholuo loanwords*. Docotorial Thesis University of Pretoria : Pretoria.

Polome , E. (1967): Swahili Language handbook. Washington: Centre for applied Linguistic.96

Schane, S. A. (1973). *Generative phonology.* Eaglewood Cliffs: Prentice Hall.99

Temu, C. (1971) The Development of political vocabulary in Swahili. In Jarida la uchunguzi wa lugha ya Kiswahili 3-5.

TUKI, (1990). *Kamusi Sanifu ya Lugha na Isimu,* Dar-es-salaam: TUKI

Verma, S. K. and Krishnaswamy, N. (1989). *Modern Linguistics*. New York: Oxford University Press.

Whiteley, H. (1969) *'Swahili –The Rise of a National Language'* Methmen. London 1969. Sura: I - IV

Zawawi, S. (1974). *Loanwords and Their Effect on the Classification of Swahili Nominals*: A Morphological Treatment. PhD Thesis, University of Columbia.

## VIAMBATANISHO

Orodho ya nomino mkopo za Kiturkana kutoka Kiswahili yaliyotumiwa katika utafiti huu

| **Kiturkana** | | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| **Othagrafia** | **Mnukuu** | **Othagrafia** |
| Abarua | [abarua] | barua |
| Asanduku | [asanduku] | sanduku |
| Agaar | [aga:r] | gari |
| Angasi | [aɳas] | ngazi |
| ngakanoi | [ ɳanɔi] | ngano |
| Asani | [asani] | sahani |
| Abakuli | [abukuli] | bakuli |
| Aleso | [alɛsɔ] | leso |
| Akaratasi | [akaratas] | karatasi |
| Acumbi | [acumbi] | chumvi |
| Atambi | [atambi] | tambi |
| Asinema | [asinema] | sinema |
| Akadi | [akad] | kadi |
| Akabati | [akabat] | kabati |
| Atinga | [ atiɳa] | tinga |

| KITURKANA | | KISWAHILI |
|---|---|---|
| **Kiothografia** | **Mnukuu** | **Kiothografia** |
| awaragat | [awaragat] | waraka |
| Abaaca | [aba:ca] | bahasha |
| Akicungi | [akicuɳi] | kichungi |
| Amutaro | [amutarɔ] | mtaro |
| Amunyororo | [amuɲɔrɔrɔ] | mnyororo |
| Awaya | [awaja] | waya |
| Emusabibu | [ ɛmusalab] | mzabibu |
| Epaka | [ ɛpaka] | paka |
| Ebei | [ɛbɛi] | bei |
| Esabuni | [ɛsabuni] | sabuni |
| Euji | [ɛuji] | uji |
| Epamba | [ɛpamba] | pamba |
| Esukari | [ɛsukari] | sukari |
| Ekazi | [ɛkas] | kazi |
| Epuko | [ɛpukɔ] | mfuko |
| Etindo | [ɛtindo] | tindo |
| Ewembe | [ɛwɛmbɛ] | wembe |
| Ejikon | [ɛjikɔ] | jiko |
| Egunia | [ɛgunia] | gunia |
| Ekawa | [ɛkawa] | kahawa |
| Ekukut | [ ɛkukut] | kuku |